

## SEMINA ZA TAASISI YA BIBLIA NA UTUMISHI: 2015

ROHO MTAKATIFU : Mwl. Steve Lancaster

(Masomo manane)

### KIPINDI CHA 1: UTANGULIZI: ROHO MTAKATIFU

Biblia inatuambia kwamba, baada ya ufuluo wake, Yesu, alioneckana kwa wanafunzi wake kwa muda wa siku arobaini – haya ni majuma sita. Mtume Paulo anatuambia Yesu alioneckana pia kwa waumini zaidi ya mia tano katika siku hizo arobaini. Matendo 1:3 unatuambia kwamba: “*Yesu, alijionyesha kwa watu hao, na aliwapa ushahidi mwangi wa kusa-dikika kwamba yeze alikuwa hai – na aliongea nao kuhusu Ufalme wa Mungu*”. Lazima kujitokeza huku kuliwasismua wanafunzi wake, kumwona Yesu akiwa hai baada ya kumwona Yesu alipokufa msalabani. Lakini Yesu alitaka kuonana na wanafunzi wake, ili kuwaandaa kwa wakati ujao; kuwatia nguvu, kuwatia moyo, na kuwambia kuhusu ufalme wa Mungu, na labda, huenda kujibu baadhi ya maswali yao.

Lakini mmeshatafakari, kwa nini Yesu hakukaa muda mrefu duniani, baada ya kufufuka kutoka wafu? Kwa nini alioneckana kwao kwa siku arobaini tu? Kwa nini Yesu hakukaa kwa miezi michache, au kwa miaka michache? Angeweza kukaa duniani kwa muda mrefu zaidi kusaidia kukua kwa kanisa. Hebu fikiria ulimwengu ungekuwaje leo, kama Yesu angekaa duniani kwa miaka elfu mbili iliyopita! Angeweza kutembelea makanisa mengi, na kuwatia moyo watu wengi, na kwa hakika, watu wengi zaidi wangemwamini kama angekaa duniani. Kwa hiyo – kwa nini hakukaa?

Basi – katika injili ya Yohana, Yesu aliwaambia wanafunzi wake, kwamba ilikuwa lazima awaache. Nahitaji kuwaacha – Yesu alisema – kwa nini? Tuangalie Yohana 14:16-17: Yesu anaongea na wanafunzi wake, katika chumba cha juu, usiku kabla hajafa: “Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwengine, ili akae nanyi hata milele; ndiye Roho wa kweli ....bali ninyi mnatambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu”. Na kisha, katika kitabu cha Yohana 16:7 Yesu anawaambia: “Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu”. Kwa nini Yesu hakukaa duniani kwa muda mrefu, baada ya kifo chake? Ni kwa sababu nyingi: Alikuwa amemaliza kazi yake maalumu; alimaliza alichokuja kukifanya. Alikufa msalabani kulipia dhambi zetu, na alifufuka kutoka kwa wafu, na alishinda kifo; kazi yake maalumu ilikwisha.

Lakini kuna sababu nyingine pia ya kwa nini Yesu aliondoka duniani na kwenda mbinguni. Yesu alipokaa duniani alikuwa na mwili tu – kama sisi. Ingawa alikuwa Mungu, pia alikuwa mwanadamu, na kwa hiyo angeweza kuoneckana kwa idadi fulani ya watu, kwa wakati mmoja. Angeweza kuhubiri kwa kundi moja la watu katika sehemu moja tu – asingeweza kuwa katika sehemu tofauti kwa muda huo huo – kwa sababu alikuwa na mwili wa mwanadamu tu. Na hii ndiyo sababu Yesu alijua kwamba ni lazima aondoche duniani, ili amtume mtu fulani, ambaye angeweza kuwa katika sehemu mbalimbali, kwa wakati huo huo.

Na tunajua kwamba ilitokea katika namna yenyepi nguvu sana, katika siku chache baadaye, Roho Mtakatifu alipokuja kwa nguvu katika siku ya Pentekoste. Yesu alipoondoka duniani, Roho Mtakatifu alitumwa kwa wanafunzi, kuendeleza kazi ambayo ameianzisha katika mioyo yao. Yesu hakuweza kuwa kila sehemu – lakini Roho Mtakatifu anaweza. Kwa namna fulani, mtu anapokuwa Mkristo; anapoweka imani yake kwa Yesu, Roho Mtakatifu huja kuishi ndani ya mtu huyo. Hili ni fumbo kubwa - na kwa akili zetu ndogo hatuwezi kuelewa hayo yame-tokeaje. Lakini, kwa imani, kwa sababu ya kile Biblia inatuambia, na kwa sababu tumezoea uwepo wake, tunajua kwamba hayo ni kweli.

Kwa nini Roho Mtakatifu ni muhimu sana? Kwa sababu bila yeye tume potea, na hatuwezi kuishi maisha ambayo Mungu anataka tuishi. Roho Mtakatifu ni muhimu kwa wokovu wetu, na ni muhimu kwa maisha ya Kikristo. Tunamhitaji atusaidie kukua, na kupevuka katika safari yetu ya maisha ya kiroho – na tunamhitaji atufundishe zaidi kuhusu Yesu Kristo. Roho Mtakatifu ni muhimu sana kwa uhai wa Mkristo, na wa kanisa pia, na ni sababu hii tutaangalia utu na wajibu wa Roho Mtakatifu, katika siku tatu zijazo.

Roho Mtakatifu ni nani? Anafanya nini? Biblia inasema nini kuhusu Roho Mtakatifu? Anafanya nini katika maisha ya Mkristo? Yesu alisema nini kuhusu Roho Mtakatifu? Kujazwa Roho Mtakatifu maana yake nini? Ni somo kuu sana, na ni muhimu sana, lakini wakati mwingine ni somo ambalo tunakaa kimya kuhusu hilo. Kwa nini? Kwa sababu tunahisi hatuwezi kutosheleza mafunzo ya kuzungumzia juu ya Roho Mtakatifu. Kwa kuwa, watu wengi kanisani, na kwa wachungaji wengi, kuna wasiwasi mwingi juu ya Roho Mtakatifu alivyo, na juu ya kazi anayofanya katika maisha yetu.

Jumapili asubuhi – mamilioni ya watu duniani kote, wanakutana kumwabudu Mungu kanisani – na wengi kati ya hao watakariri maneno ya Imani ya Mitume. Katika Kanisa la AIC, Imani ya Mitume inasemwa kila jumapili asubuhi. Imani ni orodha ya mambo yanayotuambia kanisa linacho amini, na Wakristo wamekuwa wakisema Imani hii, kwa miaka karibu elfu mbili, tangu siku za kanisa la kwanza. Mstari 1 unasema: "*Namwamini Baba Mungu Mwenyezi, Muumba wa mbingu na dunia*". Na kila mmoja wetu anaamini hivyo – kama tusingewamini Mungu Baba, tusingekuwa hapa leo! Mstari 2 unasema hivi: "*namwamini Yesu Kristo, Mwana Wake pekee, Bwana wetu*". Sisi sote hapa tunaamini kwamba Yesu alizaliwa, na kuishi duniani; tunaamini alisurubiwa msalabani, na kufa kwa ajili ya dhambi zetu, na kwamba alifufuka siku ya tatu, na sasa anakaa mbinguni pamoja na Mungu Baba. Tunamwamini Yesu. Pia inasema hivi: "*namwamini Roho Mtakatifu*". Pia ninahakika, kwamba sisi sote tunakubaliana na sentensi hii. Tunamwamini Roho Mtakatifu - au hivyo ndivyo tunavyosema tunaposoma Imani ya Mitume. Lakini, siku baada ya siku, kama tunavyoishi maisha yetu kama Wakristo na kama wachungaji – ni kweli tunamwamini Roho Mtakatifu? Na tunaamini nini kuhusu Roho? Wengine wanasema wanamwamini, lakini hawana hakika Yeye ni nani, au Anafanya nini.

Kulikuwa na muhubiri maarufu wa Kimarekani, aliyeitwa Mchungaji Tozer, ambaye alikufa karibu miaka hamsini iliopita. Ngoja niwasomee alivyosema kuhusu Wakristo na Roho Mtakatifu: "*Tunasema tunamwamini Roho Mtakatifu – lakini kama tunaamini hivyo, kwa nini mara kwa mara tunamtendea Roho Mtakatifu kama hayupo hapa kabisa? Mara kwa mara tunamuudhi; hatu-mtii, tunamzuia kufanya kazi zake, na hatu-shirikiani naye katika maisha yetu. Roho Mtakatifu amekuja kutusaidia na kutufundisha - lakini mara kwa mara tunamkataa. Anakuja kuleta nguvu, kwa sababu yeye ni Roho wa nguvu – lakini mara kwa mara tunamkataa. Roho Mtakatifu ambaye alitiia msukumo Biblia, anatutazamia kuitii Biblia, lakini kama hatuitii Biblia, tutamzimisha*".

Kwa hiyo Tozer anauliza swalii: kwa nini Wakristo wengi mara kwa mara wanamtendea Roho Mtakatifu, kama hayupo katika maisha yao? Wakristo wengine hawamjali Roho Mtakatifu; Wachungaji wengine hawamjali Roho - na hawasemi chochote kuhusu yeye – ni kama hayupo hai. Lakini kuna Wakristo wengine ambao pia wanasema mno kuhusu Roho Mtakatifu, na baadhi yao wanavyosema si kama ambavyo Biblia inatufundisha kuhusu Roho Mtakatifu. Kwa ukweli, watu wengine hawazungumzi juu ya Mungu Baba, au Yesu Kristo, lakini huangalia zaidi juu ya Roho Mtakatifu tu. Na tunaweza kusema hivyo hivyo kuhusu makanisa mbali mbali. Katika makanisa mengine, Roho Mtakatifu hazungumuziwi kabisa – na katika makanisa mengine, kuna msisitizo mno juu ya Roho Mtakatifu!

Wewe ni mchungaji wa aina gani? Je, wewe ni mchungaji ambaye hazungumzii hata kidogo kuhusu Roho Mtakatifu, na asiyeamini nguvu ya Roho Mtakatifu? Au wewe ni mchungaji yule ambaye huongelea mno kuhusu Roho Mtakatifu? Kunahitaji kuwe na uwiano katika kanisa, na katika maisha

yetu. Kanisa ambalo halitambui kazi za Roho Mtakatifu ni kanisa dhaifu – na kanisa ambalo lina shauku na Roho Mtakatifu tu, pia ni kanisa dhaifu. Kunahitaji kuwe na usawa. Ngoja niwaeleze kwa kifupi kuhusu safari yangu ya maisha ya kiroho. Nilikuwa Mkristo katika umri wa miaka tisa. Nimebarikiwa sana kwamba nimekulia katika familia ya Kikristo. Wazazi wangu wote wawili, pia babu na bibi yangu, walikuwa Wakristo, na kwa hiyo, kila juma nilikwenda kanisani. Lakini kama Mkristo mchanga, sikusikia sana kuhusu Roho Mtakatifu, kwa sababu makanisa ambayo nilikwenda, hayakuzungumzia kuhusu Roho Mtakatifu. Kulikuwa na wakati nilipozoea kukaa kanisani, na niliwaangalia watu, na baadhi yao walionekana wamechoshwa. Walionekana kama hawataki kuwa pale, na hawakuonyesha shauku kwa Imani yao. Hawakuonekana kama wana maisha ya kiroho ndani yao.

Na nilifikiri mwenyewe – kunahitajika kuwe na Ukristo zaidi ya huu. Katika injili ya Yohana 10 Yesu anasema hivi: “*nilikuja ili wawe na uzima kisha wawe nao tele*”. Lakini, kwa Wakristo wachache, hawaonekani kama wana uzima; hawaonekani kama wako hai, na hawaonekani kuishi maisha yaliyo tele; wanaonekana kama kuna kitu kimepotea – na nilifikia hitimisho kwamba, labda kiungo ambacho kimepotea ni utayari wa kumruhusu Roho Mtakatifu kufanya kazi katika maisha yao. Ingawaje watu wanasesma wanamwamini Roho Mtakatifu, labda hawataki kufungua maisha yao kwake.

Nilianza kusikia kutotosheka na maisha yangu ya kiroho - na kwa hiyo, nilipokuwa na umri wa miaka thelathini, nilianza kutafuta, na kusoma, na kujifunza, kwa sababu nilitaka kujua zaidi kuhusu Roho Mtakatifu. Nilisikia njaa ya kumjua Mungu zaidi, na Yesu zaidi – na njia ambayo tuliyonayo ya kukua katika imani yetu, ni kumruhusu Roho atembee maishani mwetu, na kutufundisha mambo ya Mungu. Na huo ni wajibu mmojawapo wa Roho Mtakatifu – kutufundisha kweli kuhusu Yesu, na tutaaangalia juu ya jambo hili kwa kina zaidi katika siku zijazo. Yesu aliwaahidi wanafunzi wake kwamba angemtuma Roho Mtakatifu aishi ndani yao – na alifanya hivyo. Lakini ahadi hiyo pia ni kwa ajili yetu leo – kama waamini, tunaye Roho Mtakatifu aliyeahidiwa ndani yetu, na kwa hakika lazima tufanye kila tunachoweza ili kumjua huyu Roho Mtakatifu, na kukaribisha uwepo wake katika maisha yetu.

Ngoja nikusomee nukuu kutoka kwa mhubiri maarufu, anayeishi Marekani, jina lake ni Jim Packer, aliandika vitabu vingi, kimojawapo kinaitwa “*Piga hatua pamoja na Roho*”. Alisema hivi: “*Katika makanisa mengi, kuna upungufu wa nguvu takatifu na msisimko wa kiroho – ni maumivu kuona hili. Tunahitaji kupata picha iliyo wazi kuhusu Roho Mtakatifu. Je, tumeelewa kweli uhalisia wa kumjua Roho Mtakatifu? Mungu mara kwa mara anasema nasi, ‘mkumbuke Roho Mtakatifu’ – lakini macho yetu yapo chini sana, na tupo bize kuangaliana sisi kwa sisi, tunapiga umbeya kuhusu maisha yetu na bado hatujajua anachokifanya. Ningependa kupiga kelele sana: ‘Wakristo amkeni! Makanisa amkeni! Wachungaji amkeni. Mkumbukeni Roho Mtakatifu! Sisi Wakristo tunahitaji kuwa macho zaidi na uwepo wa utakatifu wa Mungu wetu’*”.

Ninatumaini juma hili, tunapotumia wetu muda katika kuangalia Biblia inasema nini kuhusu Roho Mtakatifu – tutapata kumjua Yeye vizuri; hapo tutajifunza zaidi kuhusu Yeye, na tutamruhusu kufanya kazi katika maisha yetu zaidi na zaidi. Na ninatumaini kwamba tutawenza kusema kwa hakika, Imani ya Mitume inavyosema; kwamba ‘*tunamwamini Roho Mtakatifu*’; wala siyo tu kwamba tunamjua, lakini kwamba hakika tunamjua.

## KIPINDI CHA 2: UTATU NA ROHO MTAKATIFU KATIKA AGANO LA KALE:

Nianze kwa kusoma ubeti kutoka kwene wimbo maarufu sana. Wimbo huu uliandikwa miaka mia mbili iliyopita na mchungaji mwingereza, ambaye alikuwa mmisionari huko India. Na dhamira ya wimbo ni Utatu Mtakatifu. Na ingawa wimbo huo uliandikwa miaka mia mbili iliyopita, bado unaimbwa duniani kote siku hizi – hata hapa Tanzania. Tazama Nyimbo za sifa, namba sita: ni wimbo mnaoujua vizuri sana. Nitasoma ubeti wa mwisho: “*Baba, Mwana, Roho, Mungu mwenye enzi. Ulivyoviumba vyote vyakusifu. Baba, Mwana, Roho, Mungu wa mapenzi. Ewe Utatu, tunakusifu*”.

Baba, Mwana, Roho - ewe Utatu tunakusifu. Na hapo ndipo tunapo hitaji kuanzia asubuhi hii. Roho Mtakatifu ni nani? Biblia inasemaje kuhusu Roho Mtakatifu? Na kuna majibu mengi – lakini ni lazima tuanze kwa kusema kuwa Roho Mtakatifu ni Mungu. Anajua yote; ana nguvu zote; huenea pote, na yeche ni sehemu ya Utatu; Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Ewe Utatu, tunakusifu. Lakini, inawezekana kukawashangaza kujua neno ‘*Utatu*’ halipatikani katika Biblia, lakini ni neno linalotumika kuelezea mafundisho, kwamba Mungu anaonekana katika nafsi tatu tofauti, na bado ni mmoja. Na bila shaka, hili ni fumbo kwetu – ni vigumu kuelewa katika akili zetu; kwamba Mungu ni mmoja - lakini pia ni nafsi tatu tofauti, katika mtu mmoja. Yeye ni tatu katika mmoja. Tunaweza kuli-elezeaje hili?

Watu wengi wamejaribu ku-ueleza ‘*Utatu*’, na idadi ya vielelezo vimependekezwa. Kwa mfano: tafakari juu ya maji. Maji yanaweza kuonekana katika kimiminika – lakini pia, yanaweza kuonekana katika bonge la barafu katika mfumo yabisi – kama juu ya Mlima Kilimanjaro. Lakini pia, yanaweza kuonekana kama mvuke. Unapo chemsha maji, unaweza kuona mvuke unapanda juu ya sufuria. Kwa hiyo, una aina tatu tofauti za maji, lakini kuna kiambato kimoja tu - maji. Mfano mwininge: Tafakari juu ya yai lililochemswa: linatengenezwa na nini? Lina ganda gumu nje. Tunapomenya ganda la nje huwa tunapata yai-jeupe. Na halafu, katikati tuna kiini cha njano. Vitu vitatu vyote vinahitajika ili yai likamilike. Vitu vitatu tofauti – lakini ni yai moja. Mfano mwininge: mtu mmoja anaweza kuwa na wajibu mbalimbali. Tumtumie Mchungaji kama mfano: yeye ni mume; yeye ni baba, na yeye pia ni mwana; yote katika muda mmoja – lakini yeye ni mtu mmoja. Mungu ni mmoja - lakini pia ni nafsi tatu tofauti katika mtu mmoja. Yeye ni tatu katika mmoja. Sasa, kwa kuwapeni vielelezo hivi vitatu, ninahitaji kusema kwamba havielezi kwa uhakika kabisa kuhusu Utatu – vyote vina mapungufu, lakini vinaweza kutusaidia kuelewa kidogo maana ya Utatu.

Lazima tukumbuke kwamba Mungu si kama sisi. Yeye hajawekewa mipaka ya muda na nafasi, kama sisi. Yeye habadiliki au hadhoofu kama sisi; hana ubongo mdogo kama wetu; yuko nje ya uelewa wetu; Mungu ni wa milele – na kwa sababu hiyo, kuna mambo mengi ambayo ni magumu kwetu kuyaelewa. Tunajifunza katika Biblia, kwamba Mungu anaonekana katika nafsi tatu, lakini yeye ni mmoja. Wote watatu wana wajibu tofauti wa kufanya, lakini kila mmoja ni Mungu hasa, na kwa imani, tunahitaji kukubali haya, ingawa hatuyaewi kabisa. Sielewi kila kitu kuhusu Utatu, au Roho Mtakatifu – lakini ni lazima nitii kama Biblia inavyosema, na kuamini ninayosoma.

Hebu turudi kwenye neno la Mungu – kwa sababu ingawaje neno ‘*utatu*’ halipo katika Biblia, kuna aya kadha wa kadha ambazo zinaonyesha kwamba Mungu aneonekana zaidi ya nafsi moja. Mwanzo 1:26: hadithi ya uumbaji: “*Mungu akasema, ‘tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu’*”.

Tuangalie maneno ‘*tumfanye*’ na ‘*kwa sura yetu*’. Ingawa hatujaambiwa kuna watu wangapi, maneno ‘*tu*’ na ‘*yetu*’ yanaonyesha kwamba kuna nafsi zaidi ya moja. Huo ni mstari wa kwanza tulionao katika Biblia unaoonyesha ‘*utatu*’ – Mungu katika nafsi tatu. Na ni neno lile lile limetumika katika Mwanzo 11:7: mtakumbuka hadithi ya mnara wa Babeli, watu fulani walipojaribu kujenga mnara kwenda mbinguni, na Mungu alisema hivi: “*Haya, na tushuke huko, na tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao*”. Mmegundua nini hapa? Mungu hajasema ‘*nitashuka*’,

lakini anasema, ‘tushuke’ (tu). Na kwa hiyo tena, neno dogo ‘tu’ linaonyesha kwamba Mungu ni zaidi ya nafsi moja.

Halafu katika Agano Jipy, tunaona kwamba nafsi sote tatu za Utatu zimetajwa pamoja.

Mnakumbuka Yesu alipobatizwa katika Mto Yordani na Yohana Mbatizaji? Na hivi ndivyo inavyosema katika Mathayo 3:16-17: “*na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, ‘huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye’*”. Roho wa Mungu ni Roho Mtakatifu anayeshuka kwa mfano wa njiwa (hua), anashuka juu ya Kristo, Mwana wa Mungu, na sauti kutoka mbinguni kwa Mungu Baba.

Washirika wote watatu wa Utatu wametajwa. Roho Mtakatifu ni nani? Yeye ni Mungu, naye ni sehemu ya Utatu – na ingawaje kila mara anatajwa wa tatu katika orodha: Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu; haimaanishi kuwa yeye si muhimu, au ana wajibu mdogo wa kufanya. Kila nafsi katika Utatu ni sawa, na kwa hiyo Roho Mtakatifu anastahili usikivu na upendo wetu, pamoja na ibada yetu pia.

Lakini, vipi kuhusu Roho Mtakatifu katika Agano la Kale? Hatuna taarifa nyingi kuhusu Roho Mtakatifu, katika Agano La Kale, kama tulizo-nazo katika Agano Jipy, kwa sababu anatokea mara chache tu, na uchungaji wake hauelezwi katika ukamilifu. Mara ngapi unafikiri neno ‘Roho Mtakatifu’ limetumika? Linatokea mara tatu tu katika kitabu chote cha Agano la Kale – mara tatu tu. Katika Zaburi 51 na Isaya 63: Kumbuka, kwamba Mfalme Daudi alimtenda dhambi Mungu kwa kuzini na Bathsheba, na pia aliamuru Uriah mumewe auawe. Zaburi 51 ni ombi la kutubu kwa Daudi baada ya matukio hayo. Na aliomba hivi katika mstari 11: “*Usinitenge na uso wako, wala Roho yako Mtakatifu usiniondolee*”. Na katika Isaya 63 nabii unafikiri juu ya tabia za Waisraeli, walipoongozwa na Musa katika jangwa. Alisema, katika sura 63:10: “*Wakaasi, wakamhuzunisha Roho wake Mtakatifu*”. Kwa maneno mengine, walimkasirisha Roho Mtakatifu - walimhuzunisha. Na tutaona katika kipindi cha kesho, kwamba tunaweza kumsikitisha Roho Mtakatifu kwa sababu ya matendo na mawazo mabaya. Anachukizwa na kukasirishwa tunapofanya na kusema mambo yasimpendeza Mungu, na tusipo mruhusu yeye kuwa na mamlaka katika maisha yetu. Na pia Roho Mtakatifu imetajwa sura 63:11: “*Yuko wapi yeye aliyetia kati yao Roho yake Mtakatifu*”?

Lakini, ingawaje maneno ‘Roho Mtakatifu’ yanaonekana mara tatu tu katika Agano la Kale, hii haimaanishi kwamba Roho Mtakatifu alikuwa hafanyi kazi wakati huo. Alikuwa anafanya kazi kabisa - na kuna aya kadha wa kadha ambazo tunamwona akiitwa ‘Roho’, kwa herufi kubwa ‘R’. Hata mwanzoni mwa Biblia, katika sura ya kwanza ya kitabu cha kwanza, ametajwa. Mwanzo 1:2: “*Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji*”. Popote neno ‘Roho’ linapoandikwa kwa herufi kubwa mwanzoni, humaanisha Roho Mtakatifu. Kwa hiyo tunamwona Roho Mtakatifu alikuwapo hapo mwanzo; alihusika katika uumbaji wa ulimwengu. Lakini, kutajwa mara ya kwanza kwa Roho Mtakatifu akija juu ya mtu, kunapatikana katika kitabu cha Kutoka. Mungu anasema na Musa juu ya ujenzi wa hema la kukutania, na alimwambia Musa kwamba amekwisha mchagua mtu atakeyesimamia kazi hiyo, jina lake Bezaleli – Mungu alimchagua na kumtayarisha kufanya kazi.

Alifanyaje? Nitasoma katika kitabu cha Kutoka 31:2-3: “Angalia, nimemwita kwa jina lake Bezaleli mwana wa Uri, nami nimemjaza Roho ya Mungu, katika hekima, na maarifu, na ujuzi, na mambo ya kazi ya kila aina”. Bezaleli alipewa ujuzi na uwezo kufanya kazi, kwa sababu Mungu alimjaza Roho Mtakatifu. Pia tumeambwa katika Kitabu cha Hesabu, kwamba Musa alikuwa na Roho juu yake – hivyo ndivyo alivyoweza kuwaongoza Waisraeli jangwani kwa miaka arobiani.

Katika Kitabu cha Waamuzi tunaona kwamba Roho alipewa kwa watu, kama Samsoni na Gideoni, ili watiwe nguvu ya kufanya kazi zao. Mungu aliwateua na aliwapa nguvu kupitia Roho Mtakatifu, ili wafanikishe kazi hizo. Katika kitabu cha Waamuzi 6:34, tunasoma kwamba: “*Roho ya Bwana ikaja*

*juu yake Gideoni*". Katika Waamuzi 14:6 tumeambiwa kwamba: "Roho wa Bwana akaja juu yake Samsoni kwa nguvu, hivyo alimraru simba kwa mikono yake tupu"! Mtu anawezaje kumraru simba kwa mikono yake tu?! Kwa nguvu zake, Samsoni asingeweza, lakini kwa kupewa nguvu na Roho, aliweza – alipewa nguvu za rohoni.

Vipi kuhusu Mfalme Sauli? Kabla hajawa mfalme wa kwanza wa Israeli, kitu fulani kilimtokea ambacho kilimsaidia katika kazi zake. Katika Kitabu cha 1 Samueli 10:10 unasema: "Basi, walipofika Gibe, tazama, kikosi cha manabii wakakutana naye; kisha Roho ya Mungu akamjilia kwa nguvu, naye akatabiri kati yao". Kwa maneno mengine, aliwezeshwa na Roho Mtakatifu kumsifu na kumwabudu Mungu kwa shauku kubwa. Kwa bahati mbaya, miaka michache baadaye, kwa sababu ya tabia ya Sauli, tunasoma kwamba "Roho wa Bwana alikuwa amemwacha Sauli". Katika jambo hili, Mungu alimpaa Roho Sauli - lakini baadaye alimwondolea Roho maishani mwake (1 Samueli 16:14)

Baada ya Sauli, ni nani alikuwa mfalme? Mfalme maarufu sana wa Israeli – Daudi. Tumeambiwa katika 1 Samueli 16:13 kwamba nabii Samueli akamtia Daudi mafuta, na: "tangu siku hio, Roho wa Bwana akamshukia Daudi kwa nguvu". Sasa tunajua kwamba Daudi pia alifanya makosa machache maishani mwake, lakini mbali na hayo yote, alikuwa Mfalme mzuri aliyeiongoza Israeli vizuri – kwa sababu Roho alikuwa juu yake. Ngoja niwape mfano moja wa jambo ambalo Daudi aliweza kulifanya kwa sababu ya Roho Mtakatifu: Katika Kitabu cha 1 Mambo ya Nyakati 28:12 tunaona kwamba Daudi alimpaa Sulemani mwanae mpango wa kujenga hekalu jipya, lakini mpango huo haukutoka katika mawazo ya Daudi, ulitoka kwa Roho Mtakatifu. Inasema hivi: "na mfano wa yote aliyokuwa nayo kwa Roho, katika habari ya nyua za nyumba ya Bwana". Mnaona nini kinatokea hapa? Roho Mtakatifu anamsaidia Daudi anafanya mpango wa kujenga hekalu. Roho yuko juu ya Daudi akimsaidia kukamilisha majukumu aliyompa. Kwa hiyo, katika Agano la Kale, Roho Mtakatifu alikuja kwa nguvu juu ya watu, ili kuwasaidia kufanya mambo, ambayo hawakuweza kufanya kwa nguvu zao wenyewe. Roho alitolewa ili kuwasaidia watu hawa kuongoza watu wa Mungu. Zaidi ya watu ambao Roho Mtakatifu alishuka juu yao, walikuwa ni viongozi, manabii, makuhani na wafalme.

Watu kama Musa, Joshua, Gideoni, Daudi, Danieli, Ezekiel, na Isaya. Watu hawa walikuwa na nguvu za Roho juu yao, na kwa sababu ya hayo, walikuwa na uwezo wa kuongoza, na kuongea kama Mungu alivyo waambia kusema. Lakini, zingatia hili – katika Agano la Kale, Roho alitolewa kwa watu wachache tu. Kama ukiwachanganya wote pamoja, kuna watu kama mia moja, waliokuwa na uzoefu na nguvu ya Roho Mtakatifu maishani mwao. Lakini kuna unabii mmoja mwishoni mwa Agano la Kale, unaotuambia kubadilika kwa mambo. Nabii Yoeli alikuwa na habari muhimu ya kutuambia. Mwangalie katika Kitabu cha Yoeli 2:28-29: hii ni ahadi ya Mungu kwa watu wa Israeli – lakini pia, ni ahadi ambayo inatuhusu sisi.

Mungu anasema: "Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina Roho yangu juu ya wote wenyewe mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, nitamimina Roho yangu". Katika siku za Agano la Kale, Roho alikuja juu ya watu wachache tu, ili kuwawezesha kufanya kazi muhimu, lakini Mungu anasema, muda utafika ambapo Roho Matakatifu atashuka juu ya aina zote za watu; si kwa makuhani, wafalme na manabii tu, bali juu ya watu wote waaminio. Yoeli aliandika maneno hayo miaka mia tisa kabla hayajatimia! Lini yalitimia kwa mara ya kwanza? Katika siku ya Pentekoste – katika sura 2, ya kitabu cha Matendo, Roho Mtakatifu aliposhuka kwa nguvu juu ya wanafunzi.

Unaona, unapokuja katika kurasa za Agano Jipya, Yesu unapokuja duniani, tunaanza kusikia zaidi kuhusu Roho Mtakatifu. Kwa kweli, Yesu alipoondoka duniani na kupaa mbinguni – tunasikia sana juu ya Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani ya wanafunzi. Lakini – hii ni habari njema kwetu. Katika Agano Jipya, si tu Roho Mtakatifu anamwagwa juu ya watu wanaomwamini Yesu, bali, pia Roho

Mtakatifu anakuja kukaa ndani ya watu wote wanaomwamini Yesu. Na baadaye, tutaangalia kuhusu Roho Mtakatifu katika Injili, hasa katika Luka.

### KIPINDI 2 MASWALI

1. Mstari gani wa kwanza katika Biblia ambao unaonyesha nafsi tatu za Utatu zikifanya kazi pamoja?
2. Unaweza kufikiria mstari mwingine katika Injili ya Mathayo ambapo kila muhusika wa Utatu ametajwa?
3. Mara ngapi katika Agano la Kale maneno ‘Roho Mtakatifu’ yametajwa? Mara hayo tunayapata wapi?
4. Katika Kitabu cha Kutoka tunaambiwa kwamba Roho alikuja juu ya mtu fulani kumwezesha kujenga hema takatifu – mtu huyo alikuwa nani?
5. Roho alishuka kwa nguvu juu ya watu zaidi ya mia moja katika Agano la Kale.
6. Je, unaweza kutaja majina manane ya baadhi yao?
7. Kuna tofauti gani juu ya unabii wa Kitabu cha Yoeli?

### KIPINDI CHA 3: ROHO MTAKATIFU KATIKA INJILI – HASA KATIKA LUKE

Asubuhi hii, tuliona kwamba katika Agano La Kale, Roho Mtakatifu ameonekana wakati baada ya wakati, lakini kazi na wajibu wake, hazielezwi kiundani. Hatujaambiwa mengi juu ya Roho Mtakatifu ni nani, au anaonekanaje. Tuliangalia kwa kifupi mistari hiyo katika Yoeli 2 – Mungu alipoahidi kumtuma Roho wake kwa watu wote; si kwa wafalme, makuhani na manabii tu – lakini kwa watu wa kawaida walio mfuata Mungu – watu kama mimi na wewe. Alisema nini? “*Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina Roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, nitamimina Roho yangu*”. Na tunajua kwamba unabii huu umekuwa kweli katika kitabu cha Matendo, katika siku ya Pentekoste, zaidi ya miaka mia tisa baada ya Yoeli kutoa unabii – Roho Mtakatifu alipomiminwa kwa nguvu juu ya wanafunzi. Na tutaangalia kuhusu hilo baadaye.

Tunapokuja katika Agano Jipyä tunakuwa na habari nyingi kuhusu Roho Mtakatifu, na mambo mengi zaidi yanayomweleza kuwa yeye ni nani. Tunajifunza kwa undani kuhusu tabia yake, na utu wake katika Agano Jipyä. Tunajifunza alivyofanya kazi katika kitabu cha Matendo, na tunaona kazi alizofanya maishani mwa waamini, katika barua za Agano Jipyä na Injili. Nilipokuwa nikitayarisha mazungumzo haya, niliamua kutafuta ni mwandishi gani wa injili amemtaja Roho Mtakatifu zaidi, na unafikiri alikuwa nani huyo?

Basi – Marko alimtaja Roho Mtakatifu mara sita tu. Mathayo alimtaja Roho Mtakatifu mara kumi na moja. Luka alizungumzia Roho Mtakatifu mara kumi na sita, na katika Injili ya Yohana, Roho Mtakatifu ametajwa mara kumi na saba. Inavutia, tunapofika katika kitabu cha Matendo kuona kuwa, Roho Mtakatifu ametajwa mara hamsini na tano! Na, ni nani ameandika kitabu cha Matendo? Daktari Luka, ndiye mwandishi wa injili ya Luka. Kwa hiyo – taarifa zetu nyingi kuhusu Roho Mtakatifu, katika Injili, zinatoka kwa Luka na Yohana, na pia inawezekana kesho, tutaona Yesu alisemaje kuhusu Roho Mtakatifu, aliposema na wanafunzi wake, katika chumba cha juu.

Lakini kwa sasa, tuangalie katika kitabu cha Luka, kwa sababu katika sura nne za kwanza, Roho Mtakatifu ametajwa mara kumi na mbili – na katika sura mbili za mwanzo, tunakutana na watu sita ambao wamejazwa Roho Mtakatifu, na watu wa nne kati ya hao ni watu wa kawaidi sana – na kupitia hao, tunajifunza Rojo Mtakatifu alivyofanya kazi katika maisha yao.

Angalia katika Luka 1. Sasa, najua kwamba Yohana Mbatizaji hakuwa mtu wa kawaida - alikuwa nabii, lakini kuna jambo lisilo la kawaida kuhusu Yohana ambalo limetajwa katika Injili ya Luka. Katika sura hii ya kwanza kuzaliwa kwa Yohana kulitabiriwa. Malaika alimtokea Zakaria alipokuwa akifanya kazi hekaluni, na alimwambia kwamba mke wake Elizabeti atachukua mimba na atazaa mtoto mwanamume. Tunaifahamu habari hii vizuri – lakini wakati mwingine tunasahau muujiza huu ulikuwaje. Katika sura 1:7, tuliambiwa kwamba Elizabeti hakuwa na watoto; kwa maana alikuwa tasa – na pia tumeambiwa kwamba: “*wote wawili walikuwa wazee sana*”. Biblia haituambii walikuwa na umri gani, lakini wataalamu wamesema kwamba, labda inawezekana walikuwa na miaka kama 80 hivi! Kuwa na mtoto katika umri huo ni mwujiza! Hili linawezekana kwa Mungu tu. Lakini, angalia malaika alivyosema na Zakaria katika Luka 1:15, kuhusu Yohana. “*Naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mama yake*”. Na hii ni mara ya kwanza Roho Mtakatifu anatajwa katika Injili ya Luka – lakini huu ni mstari wa kushangaza!

Na bila shaka utaibua maswali mengi. Kanisani kila wakati tunawaambia watu kwamba huwezi kuzaliwa ukiwa Mkristo – kwa kweli, Yesu anasema kwamba tunahitaji kuzaliwa mara ya pili ili kuwa Wakristo – lakini hapa katika Luka 1, tutaona kwamba Yohana alijazwa Roho Mtakatifu alipokuwa tumboni mwa mama yake. Yohana ni mtu pekee katika Biblia ambaye ameonyeshwa kuwa na Roho Mtakatifu tangu kuzaliwa. Alikuwa mtu tofauti sana na watu waliomzuguka; aliteuliwa na Mungu kutayalisha njia kwa ajili ya Masiya. Na alipokuwa na umri wa miaka thelathini alianza kuwashubiria watu, akiwaita watubu. Lakini, ingawa alijazwa Roho Mtakatifu, hakuweza kufanya miujiza yoyote, kadri tunavojua, lakini Roho Mtakatifu alimwezesha kuhubiri kwa njia ambayo iliwashawishi watu watubu.

Kutajwa kwa Roho Mtakatifu kunakofuatia kunakuja sura ile ile na kunahuisha kujitokeza kwa malaika mwingine. Tazama Luka 1:35: wakati huu kuzaliwa kwa Yesu kumetabiriwa kwa Mariamu. Sasa, ukilinganisha na Elizabeti hii ni hadithi tofauti kabisa. Elizabeti ni mwanamke mzee sana – Mariamu ni mwanamke kijana, labda miaka kama 15 hivi. Elizabeti ameolewa – Mariamu hajaolewa. Yeye amechumbiwa lakini kwa wakati huu alikuwa hajaolewa na Yusufu – na kuwa na mimba nje ya ndoa ilionekana kuwa ni aibu. Elizabeti atamzaa Yohana Mbatizaji; nabii ambaye atamtengenezea njia Yesu – na Mariamu atamzaa Yesu, Masiya, Mwana wa Mungu. Haya yote yalitokeaje? Kupitia Roho Mtakatifu. Angalia katika mstari 35: “*Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli*”. Kwa hiyo hapa, ni Roho Mtakatifu ndiye anayefanya hili kutokea. Roho Mtakatifu alisababisha Mwana wa Mungu kutungwa ndani ya mwili wa Mariamu. Lakini, turudi kwa Elizabeti, binamu yake Mariamu. Tuangularie katika sura 1:41: Mariamu alikwenda kumtembelea Elizabeti, na alipoingia nyumbani, alimsalimu Elizabeti.

Mstari 41: “Ikawa Elizabeti aliposikia kule kuamkia kwake Mariamu, kitoto kichanga kikaruka ndani ya tumbo lake; Elizabeti akajazwa Roho Mtakatifu”. Elizabeti akajazwa Roho Mtakatifu. Na katika mstari 42, unatuambia kwamba alipiga kelele kwa sauti kubwa: “Umebarikiwa wewe katika wanawake, naye mzao wa tumbo lako amebarikiwa”. Roho Mtakatifu ndani yake, alimsababisha kutamka baraka kwa Mariamu, na alimsaidia kuona kwamba mtoto yule ambaye Mariamu anamchukua ni Mwana wa Mungu. Roho Mtakatifu alimpasha habari kwamba asingewenza kujua peke yake. Lakini, kuna mtu mwingine ambaye amejazwa Roho, mara tu baada ya matukio haya. Hebu angalia Luka 1:67 tunaambiwa kwamba Zakaria mwenyewe pia sasa amejazwa Roho Mtakatifu, na matokeo yake ni nini? Alianza kuimba wimbo wa kumsifu Mungu kwa yote yaliyotokea. Wimbo aliouimba Zakaria uliletwa na ulihamasishwa na Roho Mtakatifu na ultungwa na Roho Mtakatifu. Na mara nyingi, watu wanapojazwa Roho Mtakatifu, kuna wanaotamani kupiga kelele kwa nguvu, au kuimba sifa za Mungu.

Lakini, Luka hajamaliza bado, kwa sababu anataka kututambulisha kwa mtu mwingine aliyejazwa Roho Mtakatifu. Fungua sura 2:25-27: Hii ni siku ya nane baada ya Yesu kuzaliwa. Mmoja wapo

anaweza kunisomea? "Na tazama, pale Yerusalemu palikuwa na mtu, jina lake Simeoni, naye ni mtu mwenvye haki, mcha Mungu, akiitarajia faraja ya Israeli; na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake. Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti kabla ya kumwona Kristo wa Bwana. Basi akaja hekaluni ameongozwa na Roho". Na tunaambiwa kwamba Simeoni, alimchukua mtoto Yesu mikononi mwake na kumsifu Mungu. Mara tatu katika mistari mitatu, Roho Mtakatifu ametajwa. Roho Mtakatifu alikuwa amenena maishani mwa Simeoni, akimwahidi kuwa angemwona Masiya, na alikuwa ni Roho Mtakatifu aliyemhimiza na kumshauri Simeoni kwenda hekaluni, kwa wakati mwafaka, ili aweze kukutana na Yesu.

Roho Mtakatifu huongea – na Roho Mtakatifu hutia moyo - huhimiza. Je, umeshahimizwa, au kutiwa moyo na Roho Mtakatifu kufanya kitu fulani, au kusema jambo fulani? Labda, ndani yako kuna hisia inayokusukuma au kukulazimisha kufanya kitu; unajisikia kulazimishwa kufanya jambo fulani. Hivi ndivyo mara kwa mara Roho Mtakatifu huongea maishani mwetu. Huwa tunafanya nini tunaposikia, au tunapohisi vichocheo hivyo? Labda, huenda tunadharau uchochezi wa Roho Mtakatifu, na tunalizimisha lile ambalo Roho anataka kufanya maishani mwetu. Au huwa tunatii na kufanya kile ambacho Roho Mtakatifu anatutaka tufanye, ingawaje huenda tusijue maana yake nini kwa wakati huo. Na nina hakika kwamba wengi kati yenu, mnaweza kuniambia mnapohisi na kuongozwa na Roho Mtakatifu kufanya kitu fulani.

Na hapa katika Luka 2, Simeoni alihisi kuongozwa na Roho Mtakatifu kwenda hekaluni kwa wakati huo. Alimtii Roho, na alimkuta Masiya aliyeahidiwa, na baadaye, bila shaka, alikwenda nyumbani akimsifu Mungu. Kwa kweli, tunaona katika Luka 2:29-32, kwamba Simeoni anaongea maneno maalumu ambayo ni lazima atakuwa amepewa na Roho Mtakatifu – kwa sababu, Simeoni, anaweza kuona kwamba Yesu angeweza kuleta wokovu kwa watu duniani pote. Akiwa amechochewa na Roho Mtakatifu, anakwenda hekaluni, na akichochewa na Roho Mtakatifu, Simeoni, anaongea maneno ya kumsifu Mungu.

Baadaye hatusikii kuhusu Yesu kwa miaka thelathini – isipokuwa katika tukio moja ambalo tunataarifiwa katika Luka 2, mahali ambapo Mariamu na Yusufu walitembelea Yerusalemu katika Sikukuu ya Pasaka pamoja na Yesu na wakampoteza Yesu huko. Baada ya siku tatu, walimkuta hekaluni akiongea na waandishi - na tunaambiwa kwamba walishangazwa na ufahamu na ujuzi wake. Lakini mbali na tukio hilo moja, hatusikii lolote kuhusu Yesu mpaka anapokuwa na umri wa miaka 30. Kwa nini? Kwa nini Mungu hatuambii kuhusu maisha ya Yesu alipokuwa akiendelea kukua? Kwa nini Biblia haituambii kuhusu utoto wake? Labda kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa hafanyi kazi kupitia yeye.

Yesu alikua pamoja na wazazi wake huko Nazareti, na bila shaka, alikuwa mtoto mkalimilifu, kwa sababu tunaambiwa hakukuwa na dhambi ndani yake. Lakini hata tunajua kuwa Yesu hakufanya miujiza yoyote, na hakuhubiri kwa wakati huo. Si kama Yohana Mbatizaji, ambaye alikuwa binamu yake, hatujaambiwa kwamba, Yesu alijazwa Roho Mtakatifu tangu kuzaliwa. Lakini - miaka thelathini baada ya kuzaliwa kwake, tunaambiwa juu ya wakati Yesu alipotiwa mafuta na Roho Mtakatifu. Tuangalie katika Luka 3:21-22: Hili ni tukio linaloambatana na Roho Mtakatifu, ambalo limearifia kwenye Injili zote nne; ubatizo wa Yesu. Mtu mmoja asome? "*Ikawa, watu wote walipokwisha kubatizwa, na Yesu naye amebatizwa, naye anaomba, mbingu zilifunuka; Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili, kama hua; sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe*".

Tunafikia katika hatua ambayo utumishi wa Yesu unakaribia kuanza. Aliondoka nyumbani kwao Nazareti, aliwaacha wazazi wake, kaka na dada zake, aliacha kazi yake ya seremala, na alikaribia kuanza utumishi wake – alikaribia kuanza safari ambayo itaishia msalabani. Lakini - kabla hajawenza kuanza utumishi wake, kuna jambo linalo-hitajika kumtokea Yesu. Kuna kitu ambacho anahitaji kuwa

nacho maishani mwake - ili aandaliwe kufanya utumishi wake. Kulikuwa na mamia ya watu kwenye kingo za mto, waliokuja kwa Yohana Mbatizaji, ili wabatizwe – na kisha, Yesu alimsogelea Yohana Mbatizaji na kumwomba ubatizo. Kumbuka kwamba ubatizo wa Yohana ulikuwa ubatizo wa toba, lakini - Yesu hakutenda dhambi yoyote. Hakuhitaji kubatizwa kwa sababu hiyo.

Lakini alihitaji kubatizwa kwa sababu nyine. Alipoibuka kutoka majini kitu ambacho si cha kawaida kilitokea. Yesu alisimama na kuomba, na alipokuwa akifanya hivyo, Yohana aliona kitu fulani angani, na kilishuka chini taratibu mpaka kikatua juu ya kichwa cha Yesu. Huyu alikuwa ndege, hua. Kwa kweli, huyu alikuwa hua kutoka mbinguni, alama ya Roho Mtakatifu akimshukia Yesu. Hivyo ndivyo sura 3:22, inavyosema: "*Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili kama hua*". Na Yohana Mbatizaji, alijua hili lilinamaanisha nini, kwa sababu Mungu alimwambia kwamba, siku moja, atambatiza mwanamume mmoja, na atamwona akitiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu.

Katika Yohana 1:33 tunasoma maneno haya: Huyu ni Mungu anayeongea na Yohana: "*Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu*". Na tukio hili linapotokea, unabii mwiningi wa Agano la Kale unatimia kweli. Isaya 11:2 unasema hivi, unapozungumza juu ya Masiya mwahidiwa: "*Roho ya Bwana atakaa juu yake*". Lakini, sikilizeni Isaya 42:1 kwa sababu maneno hayo yako sawa sawa, na maneno ambayo Mungu aliyatumia, Yesu alipokuwa anabatizwa. Hivi ndivyo Isaya alivyosema, miaka 700, kabla ya ubatizo wa Yesu: "*Tazama mtumishi wangu; mteule wangu ambaye nafsi yangu; imependezwa naye nimetia Roho yangu juu yake*'. Na ni katika Luka hii sura 3, Yesu anapobatizwa, Yohana anaona unabii wote ukitimia. Hilo lazima lilikuwa ni jambo la kusimua kwa Yohana.

Masiya huyu mwahidiwa hakubatizwa kwa maji tu, bali anabatizwa kwa Roho Mtakatifu. Mungu Baba alimtia Yesu mafuta kwa Roho Mtakatifu – kwa nini? Kwa kazi ya nguvu na mamlaka. Utumishi wa Yesu umeshaanza, na kwa sababu alikuwa mwanadamu, alihitaji nguvu kutoka mbinguni ili kumwezesha kufanya utumishi wake. Na baada ya ubatizo wake, jinsi tunavyosoma zaidi katika Injili, mara nydingi tunaona kirai hiki kikitajwa: "*Yesu, amejazwa Roho Mtakatifu*" au "*Yesu, katika nguvu ya Roho Mtakatifu*" – na, ni mara hii tu, kwamba Yesu anaanza kufanya miujiza. Anaanza kufufua wafu, na kuponya wagonjwa, na kuhubiri kwa mamlaka na nguvu.

Yesu hakuingia katika utumishi wake wa hadharani, mpaka alipotiwa mafuta na Roho Mtakatifu. Na hapa, kuna uhusiano muhimu na tutakachozungumzia katika kipindi kijacho. Inaonekana kwamba kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, kunahitajika kwetu ili tuweze kufanya kazi yenye manufaa kwa Yesu Kristo, katika utumishi wetu. Hebu tuwatafakari wanafunzi wa Yesu – Yesu alitumia miaka mitatu kuwafundisha kuwa watenda kazi wake, lakini anawaambia, kabla hajapaa kwenda mbinguni, ni lazima wasubiri Yerusalemu wapate kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, kabla hawajaanza kazi hiyo.

### **KIPINDI 3 – MASWALI**

1. Roho Mtakatifu ametajwa mara nydingi katika Injili fulani? Na ni Injili gani hiyo?
2. Kitabu gani katika Agano Jipyä kinachozungumzia sana kuhusu Roho Mtakatifu?
3. Unafikiri unaweza kuzaliwa na Roho Mtakatifu akiishi ndani yako?
4. Katika Luka, sura ya pili, tunasoma kwamba Simioni alishawishiwa na Roho Mtakatifu anende hekaluni. Unakumbuka wakati ambapo ulihisi kushawishiwa kufanya kitu fulani?
5. Kitu gani kilitokea Yesu alipokuwa anabatizwa – na kwa nini jambo hili huhitajika kutokea?
6. Nabii gani katika Agano la Kale alitabiri kuhusu Roho Mtakatifu kukaa kwa Yesu?
7. Wanafunzi waliambiwa na Yesu wangoje jambo fulani Yerusalemu. Lilikuwa jambo gani? Kwa nini?

#### **KIPINDI CHA 4: Kuwezeshwa na Roho/Kubatizwa kwa Roho**

Jana tulimwangalia Roho Mtakatifu katika Agano la Kale, na pia, katika Injili, hasa katika Injili ya Luka. Katika sura mbili za kwanza, katika kitabu cha Luka, tulikutana na watu sita amba walikuwa wamejazwa Roho Mtakatifu. Mnawa-kumbuka ni wakina nani? Na sasa, kabla hatujaendelea kuangalia marejeo mengine katika vitabu vya Matendo, nataka tuangalia katika rejeo lingine kuhusu Roho Mtakatifu, katika kitabu cha Luka. Jana, tulihitimisha kwa kuangalia juu ya ubatizo wa Yesu – na tuliona Yesu alivyotayarishwa kuanza utumishi wake. Leo ninataka nianze kwa kuangalia maneno machache katika Injili ya Luka, yaliyotajwa na Yohana Mbatizaji.

Tuangalie kitabu cha Luka 3:16. Anayeongea hapa ni Yohana Mbatizaji wakati akiyaambia makundi ya watu yaliyokuwa yakimjia ili kubatizwa katika Mto Yordani. Alisema hivi: “*Kweli mimi nawabatiza kwa maji, lakini yeye (Yesu) atawabatiza kwa Roho Mtakatifu, na kwa moto*”. Na waandishi wengine wa Injili (Mathayo, Marko, na Yohana) walitumia maneno yaleyale, ingawa Marko na Yohana hawakutaja neno moto. Lakini wote waliandika maneno haya: “*atawabatiza kwa Roho Mtakatifu*”. Lakini maneno haya pia, yanatumiwa na watu wengine wawili katika Biblia – Yesu na Mtume Petro.

Hebu fungua Matendo 1:4-5 – na hapo ndipo Yesu anapotaja maneno haya: Kumbuka, kifungu hiki kiliandikwa baada ya ufufuo wa Yesu: “*Hata alipokuwa amekutana nao aliwaagiza wasitoke Yerusalem, bali waingoje ahadi ya Baba, ambayo mlisikia habari zake kwangu; ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache*”. Na kwa hiyo, Yesu anawaambia, ubatizo huu utatokea baada ya siku chache. “Mnahitaji kusubiri ili kupokea nguvu; mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu. Yohana Mbatizaji aliwazamisha kwenye maji – lakini mimi nitawazamisha katika Roho Mtakatifu”. Na, katika Matendo 11:16, Petro pia anasema maneno haya. “*Yesu, atawabatiza kwa Roho Mtakatifu*”.

Na kwa hiyo, maneno haya – “*batiza kwa Roho Mtakatifu*”, yametumika katika matukio sita kwenye Agano Jipy, lakini yanamaanisha nini hasa? Na yalimaanisha nini kwa wanafunzi? Kwa hiyo, tuanze kwa kuangalia kilichotokea, katika siku ambayo Roho Mtakatifu kwa mara ya kwanza alishuka juu ya wanafunzi. Hapo ndipo maneno ya Yohana na Yesu yalipotimia. Tuangalie katika Matendo 2:1-4: “*Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upopo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyiningine, kama Roho alivyowajalia kutamka*”.

Ni aya ya ajabu sana! Je, unaweza kupiga picha uone ilikuwaje kwa wanafunzi? Je, unaweza kupiga picha kama unapotafakari, kama itatokea hapa sasa? Ghafla, unatokea upopo wenye nguvu na unaovuma katika jengo; karatasi zetu zote zikatawanywa, na halafu tukaona miale ya moto ikituwa juu ya vichwa vyetu. Lakini miale hiyo isituumize wala kutuunguza – ni alama ya Roho Mtakatifu kwetu. Na kisha tukaanza kumsifu Mungu, si kwa Kiswahili, lakini kwa lugha ya ajabu ambayo hatujawahi kuitamka! Je, mnafikiri hilo lingeshangaza? Kwa hiyo – katika aya hii, kwa nini walitenda hivyo? Tuangalie mstari 4: “*Wote walijazwa Roho Mtakatifu*”. Walijazwa kwa hisia zenye nguvu ya Mungu ndani yao zisizozuilia, na walianza kumsifu Mungu kwa lugha nyiningine. Na kwa njia hiyo, kundi la watu likaanza kukusanyika – watu waliskia na kushuhudia mambo ya ajabu, na walitaka kujuu kilichokuwa kikiendelea.

Matendo 2:7 inatuambia kwamba watu walikuwa wamestaajabishwa kabisa na kilichotokea; hawakuweza kuelewa jinsi gani hawa wanafunzi waliweza kuongea katika lugha nyiningine. Watu wanaweza kuelewa yale wanafunzi wanayosema. Na bila shaka, Petro alisimama, na kueleza nini kilichotokea. Alihubiri mahubiri yake ya kwanza – yalikuwa mahubiri yenye nguvu! Tuangalie katika

Matendo 2:33: Petro akawaambia watu: “*Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia*”. Na kwa hiyo, hapa tunaona kwamba Yesu anafanya kazi ya kuwabatiza wanafunzi kwa Roho Mtakatifu. Unabii wa Yohana Mbatizaji na Yesu, sasa unatokea kweli – na wanafunzi hao hawakubatizwa kwa maji, lakini kwa Roho Mtakatifu. Kwa nini? Lengo lilikuwa nini? Na kwa nini Roho Mtakatifu alihitajika?

Muda mfupi uliopita, tuliangalia katika Matendo 1:4 Yesu alipowaambia wanafunzi wake wasiondoke Yerusalem, lakini wamsubiri Roho Mtakatifu. Aliwaahidi kwamba watabatizwa kwa Roho Mtakatifu. Tuangalie katika Luka 24:49 kwa sababu mtaona unasema karibu jambo lile lile. Hivi ndivyo Luka anavyotuambia kwamba Yesu alisema karibu na mwisho wa injili yake. “*Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu*”. Ni karibu sawa na mstari wa Matendo sura ya kwanza. Na pia tunaweza kugundua, kwa kuchunguza mistari hiyo miwili, kwamba kubatizwa kwa Roho Mtakatifu, ni sawa na kuvikwa nguvu kutoka juu – ni jambo la kuwezeshwa. Ni jambo la kujazwa nguvu ya Roho Mtakatifu, ili muwezeshwe kufanya kitu kwa Yesu. Na kwa hiyo – wanafunzi hao waliwezeshwa kufanya nini? Tuangalie katika Matendo 1:8 – na haya ni maneno ya mwisho ya Yesu kutaarifiwa duniani, kabla hajapaa kwenda mbinguni:

“Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yeruselmu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi”. Na kwa hiyo, nini kilitokea kwenye Pentekoste siku chache baadaye? Roho Mtakatifu alishuka juu yao na walijazwa kwa nguvu yake – kwa nini? Ili wawe mashuhuda wa kufaa kwa Yesu. Je, mnaona uhusiano? Hiyo ilikuwa kazi yao – Yesu anawaambia waanzishe kanisa la Kikristo, na kulisambaza duniani na kuwaambia wengine kuhusu Yesu Kristo. Alitaka wawaambie wengine kuhusu msalaba, na kuchangia injili na kila mmoja. Yesu anawateua kama watumishi wake, kushuhudia ulimwengu wote. Na bila shaka, mwishoni mwa injili ya Matayo, katika sura 28, Yesu anasema: “Enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi”. Sasa, hiyo ni kazi ngumu! Hiki ni jambo ambalo wasingeweza kulifanya peke yao. Ni kazi kubwa sana kwao kuifanya kwa nguvu zao. Lakini, Yesu anasema, msiwe na wasiwasi. Sitawaacha peke yenu kama yatima. Nitamwomba Baba amtume Roho Mtakatifu, lakini hakikisheni mnasubiri Yerusalem, mpaka mbatizwe kwa Roho Mtakatifu. Subirini mpaka mpokee nguvu hii - kwa sababu kisha, ndipo mtakuwa mmetayarishwa, na kuwezeshwa, kufanya kazi ambayo nimewapa muifanye; mtajazwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

Na kwa hiyo, zingati tena kilichotokea katika siku ya Pentekoste, wote walipobatizwa kwa Roho Mtakatifu. Matendo 2:4 unatuambia kwamba wote walikuwa “wamejazwa Roho Mtakatifu” – na hapa, ni njia nyingine tu ya kusema walikuwa “wamebatizwa kwa Roho Mtakatifu” – ina maana ile-ile. Walifanya nini? Roho aliwawezesha kuongea kwa lugha tofauti – kwa nini? Jibu - ili kundi la watu waweze kusikia habari njema ya Yesu Kristo, kwa lugha zao wenywewe. Nini kilitokea kwa Petro? Anaweza kusimama mbele ya kundi hili, na kuhubiri hubiri lake la kwanza. Sifikiri kama alikuwa na maelezo – hakuandaa mahubiri kwa wakati huo, lakini Roho alimwezesha kushuhudia. Huyu ndiye mtu, ambaye, majuma sita tu kabla, alikuwa amekana kwamba hamjui Yesu.

Kumbuka Yesu alipokamatwa na kutiwa hatiani, na Petro alipokuwa akiota moto katika behewa, na watu wachache walimuuliza juu ya kuwa mwanafunzi wa Yesu – na alijibuu mara tatu kwamba hata hamjui Yesu Kristo! Lakini sasa, yupo mbele ya kundi kubwa la watu, akihubiri hotuba yake ya kwanza, na kuwaambia watubu na kumfuata Yesu. Tofauti ni nini? Alikuwa amebatizwa kwa Roho Mtakatifu na alikuwa amepewa ujasiri wa kumshuhudia Yesu Kristo. Na matokeo yake ni nini? Nini kilitokea Petro alipohubiri hotuba yake ya kwanza? Matendo 2:41 unasema hivi: “*Nao waliopokea neno lake wakabatizwa, na siku ile wakongezeka watu wapata elfu tatu*”. Hebu piga picha, kama ingetokea kwako baada ya kuhubiri mahubiri yako ya kwanza.

Lakini – tuangalie mbele katika Matendo 4:8: Petro na Yohana walimponya kiwete hekaluni, na matokeo ya haya, kundi la watu walianza kukusanya. Na Petro alisimama na kuhubiri mahubiri mengine, na aliwaambia watu kuhusu Yesu. Viongozi wa Wayahudi waliwakamata, na kuwapeleka kwenye mahakama ya Kiyahudi na kueleza matendo yao. Na tunaambiwa kwamba Petro aliposimama kuongea alijitetea, alijazwa Roho Mtakatifu, aliongea kwa nguvu, ambayo viongozi wa Wayahudi walishangazwa na ujasiri wake. Kwa kweli tunaambiwa katika sura 4:13 kwamba viongozi walitambua kwamba Petro alikuwa mtu wa kawaida asiye na elimu - lakini aliongea kwa ujasiri sana. Kubatizwa kwa Roho Mtakatifu kunawezesha watumishi wa Mungu kufanya utumishi wao vizuri.

Katika kitabu chote cha Matendo, tumesoma kwamba mitume na wanafunzi, pamoja na wafuasi wengine wa Yesu, walipokuwa wamebatizwa kwa Roho Mtakatifu, waliwezesha kufanya mambo ambayo kwa kawaida binadamu asingeweza kuyafanya. Miujiza na uponyaji ulifanyika, na watu walinen Neno la Mungu kwa ujasiri, na watu kama Stefano alipewa nguvu ya kukabiliana hata na kifo chake, kwa sababu ya nguvu ya Roho Mtakatifu juu ya maisha yake. Katika Matendo sura ya saba, Stefano alikamatwa, na kuwekwa mbele ya mahakama ya Kiyahudi. Aliwaambia kuhusu Yesu, lakini watu walimkasirikia sana na walitaka kumuua.

Matendo 7:58-60: "*Wakamtoa nje ya mji na wakampiga kwa mawe. Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba akisema 'Bwana Yesu, pokea roho yangu'. Akapiga magoti akalia kwa sauti kuu, 'Bwana usiwahesabie dhambi hii'. Akiisha kusema haya, akafa*". Stefano aliwezaje kutulia, alipokuwa anauawa na viongozi wa Kiyahudi wenyewe hasira? Aliwezaje kuwasamehe watu amba walimwua? Tuangalie Matendo 7:55 - hapo mtapata majibu: "*Stefano alijazwa Roho Mtakatifu*". Alimwezesha na kumtia nguvu ili afe vizuri. Mnaona, Wakristo wanapoja zwa Roho Mtakatifu, wanaandaliwa na kuwezesha kufanya mambo yasiyo ya kawaida kwa ajili ya Kristo, na watu huiona tofauti.

Na hilo haliwahu watu wa Agano Jipyu tu – linawahusu Wakristo katika miaka elfu mbili iliyopita. Labda umesikia kuhusu muhubiri maarufu wa Kimarekani aliyeitwa DL Moody. Alikuwa ni mmoja wa wainjilisti wenyewe nguvu zaidi, ambaye dunia haijawahi kuona. Alihubiri watu wengi zaidi kuliko ye yeyote aliyeishi kabla ya miaka elfu mbili – zaidi ya watu milioni kumi walimsikia akihubiri, na maelfu wakawa Wakristo kwa sababu ya utumishi wake. Alikuwa Mkristo wakati alipokuwa mvulana kupitia kwa mwalimu wake wa shule ya jumapili, na baadaye akawa mchungaji huko Chicago. Na ingawa utumishi wake ulikwenda vizuri, alijua kwamba kitu fulani kilikuwa kimekosekana, na kwa hiyo alianza kumwomba Mungu amjaze Roho wake Mtakatifu maishani mwake. Alitambua kwamba alikuwa anafanya kazi kwa nguvu zake mwenyewe, na kwa hiyo alianza kumsih Mungu amjaze Roho Mtakatifu; kwamba Mungu amwezeshe kumtumikia, na aliendelea kumwomba Mungu kwa miezi kadhaa.

Siku moja, Moody alipokuwa anatembea kwenye barabara iliyojaa watu katika jiji la New York, ghafla alijawa na hisia yenye nguvu kubwa yenye kujaa uwepo wa Mungu. Haraka haraka alikwenda katika nyumba ya rafiki yake, na alimwomba chumba ambamo angeweza kuwa peke yake. Na humo alijazwa Roho Mtakatifu, na nguvu ya Mungu ilikaa ndani yake. Kwa kweli, tukio lilikuwa la nguvu mno kiasi kwamba alifikiri atakufa, na alimwomba Mungu aondee mkono wake wa baraka! Na tangu wakati huo na kuendelea kuhubiri kwake kulikuwa na nguvu isiyo ya kawaida, na maelfu ya watu walikuja kwa Yesu. Na wakati wa utumishi wake, alitaka Wakristo wapate uzoefu wa nguvu ya Roho Mtakatifu ili wawe na nguvu ya kumshuhudia Yesu – na mara kwa mara, aliwafundisha hilo, alihubiri hilo, na aliandika juu ya hilo katika vitabu mbalimbali.

Hivi ndivyo alivyosema: "Kuna jambo kama hili kuwa, mtu kuwa na uhai tu – hawana Inguvu. Mungu amepata watoto wengi – lakini wengi wao hawana maisha kamili; hawana nguvu kwa ajili ya

huduma; hawajamwomba Roho Mtakatifu zaidi ndani yao, kwa hiyo wanapungukiwa nguvu. Tunahitaji kuomba kwamba Roho Mtakatifu aje na atupake mafuta kwa nguvu yake”.

Na kwa hiyo – asubuhi hii, tuliangalia kuhusu maneno: “ubatizo wa Roho Mtakatifu” kama yaliviyotumiwa na Yohana Mbatizaji na Yesu katika Agano Jipy. Tumeangalia nini kilitokea katika siku ya Pentekoste, na wanafunzi walibatizwaje kwa Roho Mtakatifu. Tumeona kwamba hili limetokea ili waandaliwe kumfuata Yesu. Roho Mtakatifu anatupa nguvu ya kumtumikia Mungu kwa njia iliyobora – lakini, ili hili litokee, tunahitaji kuwa na utayari kwa Roho Mtakatifu ili awe na mamlaka yote katika maisha yetu.

#### **KIPINDI 4 - MASWALI**

1. Katika siku ya Pentekoste wanafunzi walibatizwa kwa Roho Mtakatifu – kwa nini?
2. Baada ya Petro kuhubiri hotuba yake ya kwanza katika Matendo sura ya pili, watu wangapi walifanyika kuwa Wakristo?
3. Nani alimsaidia Petro kuhubiri kwa nguvu?
4. Je tunamwomba Roho Mtakatifu atupake mafuta kwa mamlaka kabla hatujahubiri?
5. Je mko tayari kumruhusu Roho Mtakatifu atawale maisha yenu?

#### **KIPINDI CHA 5: Kutembea na Roho – na kujazwa kwa Roho Mtakatifu**

Tumeangalia ahadi ya Yesu '*kubatizwa kwa Roho Mtakatifu*', na tumeona hilo lilitimia kwa mara ya kwanza katika siku ya Pentekoste. Na kama tunavyosoma katika kitabu cha Matendo tunaona linatokea tena na tena – watu wakibatizwa kwa Roho Mtakatifu kwa njia zenyne nguvu ya kuwawezesha kumtumikia Yesu vizuri. Lakini sasa, nataka tuangalie baadhi ya misemo mingine, katika barua za Mtume Paulo ambazo zimemtaja Roho Mtakatifu, na hilo linatuhusu sisi kama Wakristo wa leo. Nataka tuangalie zaidi nini maana ya '*kutembea na Roho Mtakatifu*', na nini maana ya kutii amri ya Paulo ya '*kujazwa na Roho Mtakatifu*'. Tuangalie katika Wagalatia 5:16-26. Sitaangalia aya hii kwa undani zaidi – lakini itatusaidia kulenga kwenye jambo hili zaidi.

Paulo alipoandika barua kwa Wagalatia, alitaka kulenga juu ya '*imani ndani ya Yesu tu*', na uwepo wa Roho Mtakatifu katika maisha ya waamini. Alitaka kuwaonyesha kwamba, kuwa Mkristo si kutii sharia na taratibu, bali ni kufanya yote kwa imani peke yake, na utegemezi kwa Roho Mtakatifu. Ayu iliposomwa ninatumaini umligundua mara ngapi Paulo amemtaja Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ametajwa mara 7 katika mistari hiyo 11: Ni aya ilijoja Roho Mtakatifu! Na mtaona katika mstari 22, kwamba kuna mstari maarufu kuhusu Tunda la Roho, ambao tutatazama kesho asubuhi.

Paulo ametuamuru tufanye nini, hapa katika Wagalatia 5? Ametuambia kwamba, "*tukiishi kwa Roho na tuenende kwa Roho*". Tunahitaji kuongozwa na Roho, na tunahitaji kuishi kwa Roho Mtakatifu. Kwa maneno mengine, tunahitaji kuwa watu ambao tumejazwa Roho Mtakatifu. Na kama tumejazwa Roho Mtakatifu, tutaweza kupingana na dhambi, na tutaweza kuwa watu ambao tumetayarishwa kupenda. Tutakuwa watu ambao ni wakarimu, na wapole na wenye kiasi.

Mojawapo ya sababu ambazo kwazo kanisa la kwanza lilikua na kuongezeka, ni kwa sababu lilikuwa na watu ambao walikuwa "*wamejazwa na Roho Mtakatifu*". Unaweza kukumbuka kwamba katika kitabu cha Matendo 6:3: mitume waliliambia kanisa katika Yerusalem: "*kuwachagua wanaume saba ambao wanajilikana kuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu*". Na mistari michache inayofuata, katika Matendo 6:5 tunasoma kwamba mmoja kati ya wanaume waliochaguliwa alikuwa ni Stefano, ambaye alielezwa "*kama mtu aliyejaa imani, na aliyejaa Roho Mtakatifu*". Na msemo huo huo pia umetumika kumwelezea Barnaba katika Matendo 11.

Lakini, endapo tunafikiri kwamba hii inawahusu mitume tu, na kanisa la kwanza – basi tuangalie katika kitabu cha Waefeso 5:18, na hapa, Paulo ameliandikia kanisa la Efeso, na pia analiandikia kanisa katika historia yote. Anasema hivi: “*Kuweni makini mnavyoishi, si kama watu wasio na hekima, bali kama wenyewe hekima; msiwe wapumbavu, bali mwelewe mapenzi ya Mungu ni nini; msilewe kwa mvinyo, ambao unapelekea tabia mbaya, lakini badala yake, mjazwe kwa Roho*”. “Kutembea pamoja na Roho” na “kujazwa kwa Roho”. Misemo hiyo hasa ina maana gani? Kama ningekuuliza wewe leo, ‘*wewe ni Mkristo ambaye umejazwa na Roho Mtakatifu*’, ungejibu nini? Je, umekuwa mtii kwa amri ya Paulo ya kujazwa kwa Roho Mtakatifu?

Nafikiri kwamba, wengi wetu tunaona maswali hayo ni magumu kujibu – labda kwa sababu mara kwa mara kuna wasiwasi na mabishano yanayoizunguka misemo hiyo. Kwa baadhi ya watu, tunapozungumza kuhusu kujazwa kwa Roho, kitu cha kwanza kinachokuja akilini mwao, ni aina fulani ya mkutano ambapo watu wanapokutana huanza kutetemeka, na kutikisika, na kulia, na wakati mwininge kuanguka na kuongea kwa lugha tofauti.

Tuliangalia kilichotokea katika siku ya Pentekoste - katika kipindi cha nne, ambapo tuliona kwa mara ya kwanza Roho Mtakatifu akishuka kwa nguvu juu ya wanafunzi, na mambo ya ajabu pia yalitokea. Kulikuwa na sauti ya upepo mkali ulioijaza nyumba, na ndimi za moto zilikaa juu ya kila mmoja wao, lakini pia katika aya hii kuna msemo, “*wote walijazwa kwa Roho Mtakatifu*”. Kwa maneno mengine, walibatizwa kwa Roho Mtakatifu, kama Yesu alivyowaahidi. Nafikiri kwamba hilo linaweza kusababisha kuchanganyikiwa – kwa sababu tunafikiri kwamba, kila wakati tunapoona msemo “*kujazwa kwa Roho*” au “*kubatizwa kwa Roho Mtakatifu*”, hayo mambo yote ya ajabu pia ni lazima yatokee kwetu. Lakini sifikiri kwamba hiyo ni kweli. Sifikiri kwamba hivyo ndivyo Paulo alimaanisha hapa katika Wagalatia 5 au Waefeso 5.

Paulo alipoamuru kwamba tujazwe kwa Roho hapa katika Waefeso 5:18, nafikiri kwamba hili ni jambo tofauti na ‘*ubatizo wa Roho Mtakatifu*’ ambao umeelezwa katika siku ya Pentekoste. Muhubiri mzuri - Daktari Martyn Lloyd Jones, alisema kwamba tunahitaji kuelewa njia mbalimbali ambazo Roho Mtakatifu anafanya kazi. Na alisema kwamba, utendaji kazi kazi wa Roho, unaweza kugawanywa katika sehemu mbili; kazi zake za kawaida, na kazi zake zisizo za kawaida; kazi zake za kila siku – na kazi zake maalum; au kuweka hili kwa maneno mengine, kazi zake zisizo za moja kwa moja, na kazi zake za moja kwa moja. Mnaona, Roho Mtakatifu ana wajibu mwingi. Hutushawishi na kututia changamoto, na hujihusisha katika kazi ya kawaida ya kutufanya upya.

Hutubadilisha ndani yetu katika maisha ya kila siku. Mara kwa mara hatufahamu matokeo haya, kwa sababu inatoka katika kipindi cha maisha yetu. Mara kwa mara tunaita ni hatua inayo endelea ya ‘*kufanywa watakatifu*’. Njia mojawapo ambayo Roho Mtakatifu hufanya kazi ndani yetu, ni wakati tunapo soma Neno la Mungu – Biblia. Hiyo ni sehemu ya kazi yake ya kila siku, akitusaidia kuelewa na kuitekeleza Biblia katika maisha yetu. Njia nyingine ambayo Roho Mtakatifu anafanya kazi, ni njia zaidi ya njia, kwa mfano, kama alivyofanya katika siku ya Pentekoste. Hii ni njia ambayo kundi la watu, au mtu moja, anavyojazwa kwa Roho Mtakatifu, na kuwezesha na kutiwa nguvu kwa kazi, au wajibu maalum. Na hilo mara kwa mara linaweza kuambatana na uponyaji na miujiza. Kama tulivyoona katika kitabu cha Matendo, kimejaa Roho Mtakatifu akitembea katika njia zisizo za kawaida, na kuwaathiri watu kimwili, kiakili, na kiroho.

Naamini kwamba wakati mwininge Roho Mtakatifu angali anafanya kazi hivyo hata leo. Mnaweza kusoma kuhusu baadhi ya nyakati za uamusho mkuu, ambao umetoka duniani kote na katika karne zote, na pia mtasoma kuhusu Roho Mtakatifu aliposhuka katika maisha ya watu, kwa njia ya moja kwa moja, akiwawezesha kuponya wagonjwa, na hata kufufua wafu! Fikirini kuhusu Uamusho wa Afrika Mashariki, ambao ulianza miaka 85 iliyopita, ulianza kuitia mmisionari mmoja katika nchi ya Ruanda, na ulienea mpaka Uganda na Kenya, na kisha uliinga Tanzania. Roho Mtakatifu alitembea

katika njia isio ya kawaida, na maelfu ya watu waliskia hatia ya dhambi walizozitenda – na walitoa maisha yao kwa Yesu. Wakati huo Roho Mtakatifu alikuwa alitembea katika njia pekee katika Afrika Mashariki. Lakini, tunaposoma kuhusu watu kama Stefano na Barnaba ambao walikuwa “*wamejazwa Roho Mtakatifu*”, sidhani kama inarejelea utendaji usio wa kawaida wa Roho Mtakatifu. Nafikiri inarejelea utendaji wa kawaida wa Roho Mtakatifu katika maisha yao. Kila siku walikuwa wanaendelea kumruhusu Roho Mtakatifu kufanya kazi ndani ya maisha yao – wakati wote walikuwa wamejazwa Roho, na kuongozwa na Roho.

Lakini, hili maana yake ni nini – kujazwa kwa Roho Mtakatifu, kama ilivyo elezwa na Paulo? Paulo anapoamuru kwamba tujazwe kwa Roho Mtakatifu, nyakati zote, anamaanisha nini? Nitasoma tena Waefeso 5:18 katika tafsiri tofauti za Biblia, ambazo zitatusaidia kuelewa msemo huu vizuri. “*Mruhusu Roho Mtakatifu kukujaza na kukutawala*”.

Na walimu kadha wanasema kwamba, maana iliyopo nyuma ya neno ‘*kujazwa*’ - ni ‘*kutawaliwa*’. Kwa hiyo - Paulo aliposema “*kujazwa kwa Roho Mtakatifu*”, pia inaweza kumaanisha: “*jiruhusu mwenyewe kutawaliwa na Roho Mtakatifu*”. Kwa maneno mengine, katika mazingira haya, mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu ni mtu ambaye amejiruhusu mwenyewe kutawaliwa na Roho Mtakatifu. Stefano na Barnaba walikuwa watu ambao waliendelea kuathiriwa na Roho Mtakatifu; walitawaliwa na Roho Mtakatifu. Mnaona, kama mtu amejawa na hasira – halafu hasira hiyo inatawala maisha yake. Kama mtu amejawa na hofu, kwa hiyo hofu inatawala maisha yake; kama mtu amejawa ulafi – kwa hiyo ulafi unatawala maisha yake. Kama mtu amejawa na pombe – kwa hiyo kila kitu anachofanya kitakuwa kimeathiriwa na pombe hiyo. Kwa hiyo, mtu anapojazwa Roho Mtakatifu – mtu huyo anatawaliwa na Roho, na kila kitu anachofanya maishani mwake kitakuwa kimetawaliwa na Roho Mtakatifu, akifanya kazi ndani yake.

Kwa hiyo, swali ni hili tena: Umejawa Roho Mtakatifu? Je, wewe ni Mkristo unayetawaliwa na Roho? Kila siku, unashirikiana na Roho Mtakatifu, na kumruhusu akuongoze katika maisha yako – au unajaribu kufanya mambo kwa njia yako mwenyewe, na kujifanya bosi wa maisha yako? Unaona, kujazwa kwa Roho ni jambo la kushirikiana na Roho Mtakatifu. Kujazwa Roho Mtakatifu, katika Waefeso 5:18, haimaanishi hasa nina Roho zaidi ndani yangu, lakini inamaanisha kwamba Roho Mtakatifu anayo maisha yangu zaidi. Kwa maneno mengine, hatumhitaji Roho zaidi ndani yetu – lakini Roho Mtakatifu anatuhitaji zaidi tuwe tunapatikana kwake, hii ndiyo sababu amri hii endelevu inayotufanya turuhusu kujazwa kwa Roho wake kila wakati – na si katika wakati mmoja.

Kwa namna moja, Wakristo wote wa kweli tayari wamekwisha kuwa na Roho Mtakatifu maishani mwao. Roho Mtakatifu anakuja kukaa ndani yao mara tu wanapokuwa Wakristo. Kwa hiyo Roho Mtakatifu anaishi ndani ya waamini wote wa kweli – lakini kwa kiasi gani Mkristo anamruhusu Roho Mtakatifu kumjaza na kumtawala? Mkristo asiyi mtii, ambaye hatembe na Mungu, na ambaye anachagua kuishi maisha ya kukaidi, anamsikitisha Roho Mtakatifu – na mtu huyo hatakuwa amejazwa Roho Mtakatifu, au kutawaliwa na Roho, kama mtu ambaye anatembea karibu na Mungu. Mnaona, ujazo wa Roho si jambo la kujazwa, au kuwa tupu tu, kwa Mkristo. Badala yake ni jambo la kiwango, ambayo linabadilika kulingana na jinsi tunavyoshirikiana naye.

Tunamruhusu Roho Mtakatifu atawale maisha yetu kwa kiasi kikubwa namna gani? Tunawezaje kuwa watu ambao tumejawa Roho Mtakatifu? Tunawezaje kuwa watu tunaotawaliwa naye? Jibu ni rahisi kusema, lakini mara kwa mara ni vigumu kufanya kwa vitendo. Tunamruhusu Roho Mtakatifu atawale maisha yetu, kwa kiasi kikubwa, na kujiweka chini yake; na tunamruhusu kufanya namna yoyote anavyotaka katika maisha yetu. Tunahitaji kuwa na tabia ya kujiweka chini yake, na kumruhusu Mungu kufikia kila eneo la maisha yetu – lakini, shida ni kwamba, mara kwa mara, kuna sehemu za maisha yetu, ambazo zimejawa na umimi – ambapo hakuna nafasi ya Roho Mtakatifu kufanya kazi zake!

Jinsi tunavyojikabidhi kwa Mungu zaidi, na kumtii, ndivyo Roho Mtakatifu anavyoweza kutawala na kujaza maisha yetu – na ndivyo anavyoweza kututumia kwa nguvu kwa malengo na kwa utukufu wake. Haya yote ni kuhusu kuishi kwa ajili ya Yesu kila dakika, na tunavyoendelea kumtegemea, ndivyo anavyo tujaza. Tunapoendelea kutumia muda kwa kusoma neno lake, na kutumia mafundisho yake katika maisha yetu, ndipo anatujaza; na tunapojiweka chini ya kanuni yake, na kumruhusu aweze kutia njia yake maishani mwetu – ndivyo anavyotawala zaidi na kwa Roho wake wenye nguvu.

Ngoja ni jumlishe kwa kifupi: Katika Waefeso 5:18 Paulo anaamuru kwamba tujazwe Roho Mtakatifu. Hapendekezi kwamba tujazwe; anaamuru tujazwe. Amri hii siyo ya hiari; imetupasa tu kumwachia Roho Mtakatifu atujaze; hakuna matambiko au fomula inayotumika. Tunahitaji kushirikiana naye tu. Na tambua kwamba amri hii ni endelevu; siyo zoezi la mara moja tu – ni lazima tuendelee kumruhusu Mungu atujaze kwa namna endelevu.

Kwa hiyo, tusimhuzunishe Roho Mtakatifu, au kumsukumia mbali nasi; tusimwogope Roho Mtakatifu. Tuwe watu wanaomkaribisha Roho Mtakatifu katika maisha yetu; tutembee na Roho Mtakatifu, na tujazwe Roho Mtakatifu – ili tuwezeshwe kumtumikia katika utumishi wetu. Wagalatia 5:16, unasema nini? “*Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho*”.

#### **KIPINDI 5 – MASWALI**

1. Tunatembeaje na Roho?
2. Watu kama Stefano na Barnaba walielezewa kuwa ni wanaume waliojazwa Roho Mtakatifu. Je unaweza kusema kwamba umejazwa Roho Mtakatifu? Kwa nini?
3. Roho Mtakatifu anafanya kazi kwa njia zilizo za kawaida na zisizo za kawaida. Toa mfano anavyofanyaje kazi kwa njia zilizo za kawaida na anavyofanya kazi kwa njia zisizo za kawaida?
4. Tunamruhusuje Roho Mtakatifu atawale maisha yetu zaidi?
5. Tunamhuzunishaje Roho Mtakatifu?

#### **KIPINDI CHA 6: MSHAURI NA WAJIBU WAKE: YOHANA 14:15-27**

Katika kipindi hiki, tutatumia muda mwangi katika injili ya Yohana, na hasa katika sura 14. Tutaangalia ahadi ambazo Yesu alizifanya kwa wanafunzi wake kumtuma Mshauri, na jinsi tunavyozitazama ahadi hizo, tutajua zaidi kuhusu tabia ya Roho Mtakatifu, na kazi anayofanya katika maisha Mkristo. Roho Mtakatifu yukoje, na anafanya nini katika ya maisha yetu? Nafikiri kwamba ndani ya Utatu, ni Roho Mtakatifu ambaye anabaki kuwa fumbo kubwa kuliko wale wengine wawili. Katika akili zetu tuna picha ya Yesu – tunajua kwamba ingawa alikuwa Mwana wa Mungu pia alikuwa mwanadamu – na tunajua tunaposoma katika injili kwamba alitembea duniani, na alipata uzoefu wa mambo tunayofanya kama wanadamu. Tunaweza kutambua ubinadamu wake. Na tunajua kwamba katika miaka 2000 iliyopita kwa kweli watu walimwona Yesu.

Halafu kuna Mungu Baba. Na ingawaje hakuna aliyemwona Mungu uso kwa uso, tunajenga picha katika akili zetu kuhusu Mungu alivyo – tunasoma alivyofanya katika Agano La Kale, na tunafahamu juu ya utukufu na ukuu wake: Mungu wa milele ambaye alikuwepo wakati wa Uumbaji na atakuwepo mwishoni mwa wakati. Na labda tunaweza kupata sura ya Mungu Baba kwa sababu kuna uhusiano katika uzoefu wetu wa ubaba – ama sisi wenyewe kuwa mababa au tumekuwa na baba zetu wenyewe. Lakini labda huenda ikawa vigumu kwetu kupata sura ya Roho Mtakatifu. Hatuwezi kumwona Roho Mtakatifu kimwili, ingawa wakati uliopita, alijionyesha kwa maumbo mbalimbali. Tulipoangalia juu ya ubatizo wa Yesu, tuliona kwamba Roho Mtakatifu alishuka kwa umbo la njiwa

(au hua). Katika Siku ya Pentekoste Roho alitokea kama moto; ndimi za moto zilikaa juu ya wanafunzi. Na katika tukio hilo hilo alitokea kama upopo wenyewe nguvu – hiyo ndiyo njia ambayo alijionyesha. Matendo 2:2, unasema hivi: “*Kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upopo wa nguvu, ukienda kasi ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi*”. Na kwa njia nyingi, Roho Mtakatifu yuko kama upopo.

Huwezi kuona upopo, lakini unaweza kuuhisi na kuona unachofanya. Unaweza kuona miti ikitikisika upopo unapovuma kwenye matawi. Jinsi upopo unavyo vuma mara kwa mara unaweza kuona mavumbi – lakini kwa kweli huwezi kuuona upopo wenyewe. Unaweza kuona unachofanya tu. Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu – yeze ni nguvu ambayo mtu yeyote hawezi kuiona – lakini unaweza kuona matokeo ya Roho Mtakatifu katika maisha ya watu. Na matokeo hayo yote yanaweza kuwa kama upopo mwanana – au upopo wenyewe nguvu kama chamchela.

Yesu alimwambia nini Nikodemo katika Yohana 3:8? “*Upopo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho*”. Hatuwezi kuzuia au kutiisha upopo – na hivyo ndivyo alivyo Roho Mtakatifu pia.

Kwa kweli katika lugha ya Kigiriki, ambayo ndiyo lugha ya asili ya Agano Jipya, neno lililotumika kwa ‘*upopo*’ na ‘*pumzi*’, ni sawa na neno ambalo limetumika kwa Roho Mtakatifu – ni neno lililo sawa. Ni neno la Kigiriki ‘*pneuma*’. Tunapata neno ‘*pneumatic*’ kutoka neno ‘*pneuma*’ – hewa inayosukumwa kwa nguvu, kama hewa inayotiwa katika matairi. Pia tunapata neno ‘*nimonia*’ kutokana na neno ‘*pneuma*’. Huu ni ugonjwa unaoathiri mapafu na upumuaji wa mtu. Kwa hiyo neno ambalo limetumika kwa Roho, upopo na pumzi ni neno lile lile. Na tunaweza kuona uhusiano huo hata katika Agano la Kale.

Roho kwa Kiabrania ni ‘*Ruach*’, pia ni neno litumikalo kwa ‘*upopo*’ na ‘*pumzi*’. Kuna hadithi yenyenye nguvu sana katika Kitabu cha Ezekiel - Sura 37 inatuambia kuhusu bonde la mifupa mikavu. Ezekiel anasimama katika bonde, na anachoweza kuona ni mifupa pote ardhini. Lazima ulikuwa mwonekano wa ajabu; labda hata mwonekano mbaya. Mungu anaiambia mifupa, kupitia Ezekiel, “*Nitaweka pumzi ndani yenu na mtakuwa hai*”. Ni sura ya ajabu lakini yenyenye nguvu. Inatupa taswira nzuri ya kile ambacho Roho Mtakatifu hufanya katika maisha yetu. Pumzi ya Mungu; Roho wa Mungu; upopo wa Mungu unapumua katika miili yetu na tunakuwa hai kiroho. Roho Mtakatifu analeta uhai katika miili yetu, na tumefanywa hai, kwa sababu Roho Mtakatifu yumo ndani yetu. Na kunaweza kuwa na nyakati, kama ilivyokuwa katika siku ya Pentekoste, upopo ule ulipovuma kwa nguvu, na matokeo yake yana nguvu kubwa katika maisha yetu. Roho Mtakatifu; upopo wa Mungu, unakuja kwa nguvu kwa watu wake.

Lakini hebu tuangalie katika Yohana 14, ili kuona zaidi kuhusu anachofanya Roho Mtakatifu kwa waamini. Sura 13-17 zinajulikana kama sura za chumba cha juu – ni sehemu muhimu katika Biblia, mahali ambapo Yesu alitoa baadhi ya mafundisho muhimu sana kwa wanafunzi wake. Na hayo yote yalitokea saa chache kabla hajakamatwa. Katika Yohana 13:33, Yesu aliwaambia: “*Enyi watoto wadogo, bado kitambo kidogo nipo pamoja nanyi. Mimi ni endako ninyi hamwezi kuja*”. Aliwatahadharisha kwamba bado kitambo atawaacha, na hawataweza kumfuata. Kwa hiyo, Yesu, anasemaje kwao? Hebu tusome Yohana 14:15-27.

Nakaribia kuwaacha, Yesu alisema, lakini msiwe na wasiwasi, msiogope, sitawaacha peke yenu – nitamtuma Msaidizi awe pamoja nanyi. Yeye ni Roho Mtakatifu; yeye ni Roho wa kweli, na yeye ni Mshauri. Sasa, katika Biblia yangu ya Kiingereza, neno ambalo limetumika ni Mshauri, lakini najua kwamba katika Biblia zenu za Kiswahili, neno ‘*Msaidizi*’ limetumika. Baadhi ya tafsiri za Biblia zinatumia neno ‘*mfariji*’, ingawaje sidhani kwamba inaeleza kwa ukamilifu Roho Mtakatifu anavyofanya – inakosa maana. Roho Mtakatifu ni mfariji na msaidizi, lakini yeye pia ni zaidi ya hayo.

Kama mlikuwa mnasoma katika Agano Jipyä katika lugha ya asili ya Kigiriki, neno ambalo linatumika kwa *Msaidizi* au *Mshaurini* neno ‘*parakletos*’. Ligawanye neno katika sehemu mbili, na unagundua maana yake. Neno ‘*para*’ maana yake ni kama neno ‘*mbavuni mwao*’ – na neno ‘*kletos*’ maana yake ni ‘*kuita*’.

Kwa hiyo, neno hilo ‘*parakletos*’ humanisha mtu ambaye ameitwa kutembea *ubavu kwa ubavu* na mtu, kutenda kama mshauri na msaidizi wake. Ni neno ambalo mara kwa mara linapatikana katika muktadha wa kisheria. Huyu ni mtu ambaye anatetea kesi yako mahakamani; mwanasheria ambaye anasimama karibu na wewe kuwa wakili wako; mtu anayekutia moyo. Muda wowote shida inapotokea, mwanasheria huyu anaweza kuitwa, na kuja mara moja na kukupatia msaada. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo. Ni kama tuna mwanasheria maalum ambaye kila wakati yupo kutuwakilisha na kusimama mbavuni mwetu, kutusaidia katika shida zetu, kama tunavyoenenda maishani.

Lakini nataka tuone kitu kingine hapa katika mstari 17, kwa sababu ni muhimu kuona kwamba katika Agano Jipyä zima, ni wazi kwamba Roho Mtakatifu ni mtu dhahiri. Angalieni anachosema katika mstari 17: “*Ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni wala haumjui, lakini ninyi mnajua, kwa sababu anakaa kwenu naye atakuwa ndani yenu*”. Unaona nini katika mstari huo? Mara 5 Roho Mtakatifu anaonyeshwa kama ‘yeye’. Roho Mtakatifu ni mtu - yeye si kitu. Anafanya mambo ambayo yanahusiana na nafsi ya mtu. Huongoza, hufundisha, huhisi, hutafuta, huomba, hupenda, na anaweza kuhuzunishwa, anaweza kuudhiwa na kuambiwa uwongo. Ni mtu tu anaweza kufanya mambo haya; ni mtu tu anao uwezo wa kuhisi na kuathiriwa.

Turejee kwenye mstari 16, kwa sababu kuna neno Yesu analitumia, ambalo linaweza kutusaidia kumwona Roho Mtakatifu kuwa ni mtu: “*Nitamwomba Baba, na atawapa Mshauri mwingine awe nanyi hata milele*”. Angalieni neno hilo ‘*mwingine*’. Neno la Kigiriki ambalo limetumika hapa ni ‘*allo*’, na maana yake ni ‘*wa aina moja*’ – na kwa hiyo Yesu anawaambia wanafunzi wake, nitamtuma mtu mmoja ambaye yuko kama mimi – si mtu tofauti. Nitamtuma mmoja aliye kama mimi mwenyewe; mtu mmoja mwenye huruma ile ile, na upendo, na tabia bainishi za kimungu kama mimi. Yesu alikuwa msaidizi wa wanafunzi kwa miaka 3 – aliwafariji, aliwafundisha, alitembea bega kwa bega nao, au mbavuni mwao – lakini sasa, wangkuwa na msaidizi mwingine, ambaye yuko sawa sawa na Yesu kabisa – akiwasaidia kama alivyofanya Yesu. Kwa hiyo, kwa njia nyingine – kama tunataka kupata picha ya Roho Mtakatifu yukoje, tunahitaji kuangalia tu utu wa Yesu Kristo.

Na kwa hiyo, Yesu atamtuma Msaidizi acae nao – na kwa kipindi cha majuma na miezi iliyofuata, tunamwona Roho Mtakatifu akiwasaidia wanafunzi kwa njia nyingi. Mshauri huyu atakuja mbavuni mwao, kuwasaidia wanapowaambia wengine kuhusu Yesu. Atawatia nguvu wanapajaribu kupendana wao kwa wao, na atawafariji na kuwasaidia kuelewa kinachotokea. Kwa kweli, mambo muhumi ambayo Roho Mtakatifu atafanya, ni kuwasaidia kumwelewa Yesu Kristo ni nani – tuangalie mstari 26: “*lakini Mshauri huyo atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia*”. Moja ya kazi za Roho Mtakatifu, ni kuwa mwalimu kwa wanafunzi hawa.

Katika miaka 3 iliyopita Yesu alikuwa mwalimu wao – lakini kwa sababu Yesu anakaribia kuwaacha, wanahitaji mwalimu mwingine kuwasaidia kumjua Yesu ni nani. Katika miaka 3 ambayo wanafunzi hawa walikuwa na Yesu, walishuhudia baadhi ya miujiza ya ajabu sana, na pia walikuwa wamemsikia Yesu akisema mambo mengi – na baadhi ya mambo hayo hayakuleta maana yoyote kwao! Bado hawaelewi Yesu alichokuja kukifanya. Na kwa hiyo, kazi muhimu ya Roho Mtakatifu itakuwa kuwafundisha kuhusu Yesu, na mpango wa ukombozi – na kuwakumbusha yote Yesu aliyowaambia wakati wote wa utumishi wake. Kwa maneno mengine, mambo yataanza kuleta maana kadiri Roho Mtakatifu anavyokaa na kufanya kazi ndani yao. Na tunajua kwamba hayo yalitokea. Tuna maandishi ya Agano Jipyä kuthibitisha hili, kwa sababu baadhi ya wanafunzi hao waliandika na kueleza maisha

ya Yesu kwa wasomaji wao, hili ni kwa sababu waliwezesha na Roho Mtakatifu kufanya hivyo. Yesu aliwaambia wanafunzi wake “*Roho Mtakatifu atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia*”. Na kama tutamuruhusu, huyo ni moja ya wajibu anaoufanya Roho Mtakatifu katika maisha yetu, kutufundisha na kutukumbusha Yesu alivyosema na kufanya – kutusaidia kulenga zaidi kwa Yesu.

Mmoja wa wataalamu wa Biblia, anauelezea utumishi wa Roho Mtakatifu kama ‘*taa kubwa yenye mwanga mkali*’ (floodlight). Ngoja niwaeleze: Jiji la London katika Uingereza ni kubwa sana – zaidi ya watu millioni 8 wanaishi humo. Pia ni jiji kongwe, lenye baadhi ya majengo makubwa ya kuvutia. Labda mmeyaona baadhi yake katika televisheni, au katika magazeti: kuna *Jumba la Buckingham* ambapo Malkia anaishi. Na kuna ‘*Westminster Abbey*’ ambalo ni kanisa kongwe na kubwa sana. Na pia karibu na hili, kuna *Nyumba ya Bunge* – ambamo serikali ina ofisi zake. Na majumba hayo yote ni maarufu na makubwa sana, na yenye kuvutia. Na huvutia zaidi nyakati za usiku, kwa sababu taa kubwa zenye mwanga mkali huyaangazia. Taa hizi kubwa zenye mwanga, kwa kawaida ziko chini zikimulika juu kuelekea majengo, kiasi kwamba zinakuwezesha kuona majengo haya ya kuvutia, hata kama ni usiku. Ni kama mtu fulani ameshikilia tochi yenye mwanga mkali sana na kuangazia majengo hayo. Na kwa njia hiyo hiyo, moja ya kazi za Roho Mtakatifu ni kumwangaza Yesu na kumfanya aonekane. Roho Mtakatifu anajificha katika taa zenye mwanga mkali, zinazoangaza Yesu nguvu, ili tumwone vizuri na kumwelewa.

Lakini nataka tuone kitu kingine hapa. Watu wanapotembea katika mitaa ya London usiku, wanavutiwa na majengo – na siyo taa zenye mwanga mkali. Watalii hawana shauku juu ya taa zenye mwanga mkali, lakini wanashangazwa na kile kinachoonyeshwa na taa zenye mwanga mkali. Mnaona, Roho Mtakatifu haweki hajivutii mwenyewe, lakini mara zote anavuta usikivu wetu kwa Yesu. Roho Mtakatifu hataki tumwangalie yeze tu, na kushangazwa na taa zenye nguvu ambazo mara nyingi anatoa, lakini anataka macho yetu na mioyo yetu imwone Yesu. Hiyo ni kazi yake. Mbali na hayo, je mmetambua kwamba katika Biblia, Roho Mtakatifu hajaitwa ‘*mfalme*’?

Mungu Baba na Yesu Mwana, wameva taji za kifalme, na kukaa juu ya viti vya enzi, lakini siyo Roho Mtakatifu. Hatafuti kuwafanya watu wajishushe kwake, kama Mfalme anavyofanya – lakini badala yake anatafuta kuwaongoza watu wapate kujishusha kwa Baba na Mwana.

Lakini hapa kuna onyo. Roho Mtakatifu, kama mtu watatu katika Utatu, anastahili usikivu wetu, labda usikivu mkubwa zaidi kuliko tunaompa. Hatuwezi kuishi maisha ya Kikristo ya kufaa, kama hatuweki usikivu wetu kwa Roho Mtakatifu, na utendaji kazi wake – lakini Roho Mtakatifu asiwe lengo letu la kwanza. Kuna hatari katika baadhi ya makanisa, na kwa baadhi ya watu, kuweka msisitizo zaidi kwa Roho Mtakatifu, na matokeo yake, Mungu Baba na Yesu Mwana wanaachwa nyuma. Msisitizo zaidi kwa Roho Mtakatifu, na anavyofanya, unaweza kusababisha shida. Sasa, nikisha kusema hivyo, ngoja pia niseme hivi. Ingawa ni hatari kukaza zaidi juu ya Roho Mtakatifu, pia ni hatari kutosisitiza juu ya Roho Mtakatifu. Kama hatuweki usikivu wa kutosha kwa Roho Mtakatifu, na kama tunaweka msisitizo mdogo tu kwa anayofanya, imani yetu inaweza kukauka na kuwa jangwa, na wakati mwingine, tunaweza kumzimisha Roho Mtakatifu maishani mwetu.

Hisia zangu ni kwamba kunahitajika kuwa na uwiano mzuri. Tunahitaji kumheshimu na kumpenda Roho Mtakatifu – tunahitaji kumkaribisha – tunahitaji kumwabudu na kumsujudu, kwa sababu yeze ni Mungu – lakini pia tunahitaji kuwa waangalifu ili kwamba tusiweke umuhimu zaidi kwa Roho Mtakatifu, na kusahau kuhusu Mungu Baba, na Yesu Mwana. Roho Mtakatifu asingetaka hivyo, kwa sababu kama tunavyo ona, moja wapo wa wakazi zake muhimu ni kummulika Yesu, kufundisha na kutusaidia kuelewa kazi za Yesu. Sisi ni watu tulio barikiwa kabisa! Roho Mtakatifu anakuja kutufundisha, kutuongoza, kutupa maisha, wokovu na ukombozi. Anakuja kutupa uhakika wa

ukombozi, na kutembea mbavuni mwao, akiwa Msaidizi na Mfariji; anakuja ili tuweze kumwelewa Yesu na kumwabudu zaidi.

#### KIPINDI 6 – MASWALI

1. Roho wa Mungu analeta maisha – Nabii gani aliambiwa na Mungu atabiri katika bonde la mifupa mikavu?
2. Katika Kitabu cha Yohana, sura ya kumi na nne, Roho Mtakatifu ameelezwa kuwa ni nini?
3. Taja baadhi ya wajibu wa Roho Mtakatifu. Hufanya nini katika maisha ya Mkristo?
4. Kuna hatari gani katika kuweka umuhimu kupita kiasi juu ya Roho Mtakatifu?
5. Kuna hatari zipi za kutoweka umuhimu wa kutosha kwa Roho Mtakatifu?

#### KIPINDI CHA 7: ZAWADI ZA ROHO/KARAMA ZA ROHO

Katika kipindi hiki, tutaangalia kuhusu somo la Zawadi za Roho, au Karama za Roho, ambazo Paulo anazizungumzia katika kitabu cha Warumi, na Wakorintho wa kwanza. Hizi ni karama ambazo wanapewa waamini wa kweli na Roho Mtakatifu. Mnakumbuka unabii wa Yoeli? Alitabiri kwamba ungekuja wakati, ambao Mungu angeminina Roho wake kwa waamini wote – na tuliona hayo yalianza kutokea katika siku ya Pentekoste. Kama watu zaidi na zaidi walikuwa Wakristo, kanisa lilianza kukua – na tunaona kwamba Roho Mtakatifu aliminiwa kwa watu – Wayahudi wote, na wasio Wayahudi; mitume, na watu wa kawaida. Na moja ya tabia bainishi za kanisa la kwanza, ni ugawiji wa karama za Roho kwa waamini. Kwa hiyo – karama hizi za Roho ni nini, na lengo lake ni nini? Je, bado tunaona karama hizi za Roho zikitumika siku hizi?

Tuangalie katika kitabu cha 1 Wakorintho 12:1: “*Basi ndugu zangu kwa habari ya karama za Roho sitaki mkose kufahamu*”. Kwa maneno mengine, Paulo anasema, nawataka mjue kuhusu karama za Roho. Kwa nini? Kwa sababu ni muhimu sana katika kanisa. Paulo anasema, nawataka muzifahamu; na ninawataka mjue kuhusu karama hizi za Roho ambazo Roho Mtakatifu anatoa. Na kisha, tuangalie mstari 4-6: “*Basi pana tofauti za karama; bali Roho ni yeye yule. Tena pana tofauti za huduma, na Bwana ni yeye yule. Kisha pana tofauti za kutenda kazi, bali Mungu ni yeye yule azitendaye kazi zote katika wote*”. Angalieni kwa makini mistari hiyo mitatu, kwa sababu tuna wahusika watatu wa Utatu wametajwa: Roho, Bwana, na Mungu. Mstari wa nne: “*Bali Roho ni yeye yule*”. Mstari 5: “*bali Bwana ni yeye yule*”. Mstari 6: “*bali Mungu ni yeye yule*”. Tuendelee kusoma kuanzia mstari 7-11.

Kwa hiyo, karama hizi za Roho ni nini? Basi, neno ambalo limetumika kuelezea karama za Roho kwa lugha ya Kigiriki ni ‘charisma’, maana yake ni ‘karama za neema’. Na kwa hiyo, karama mbalimbali ambazo zimeorodheshwa katika aya hiyo, ni karama zote za neema. Hatustahili, lakini Roho Mtakatifu anazitoa kwetu. Zimetolewa bure kwa waamini. Hazijatolewa kama matokeo ya juhudzi zetu, na haziwezi kufanyiwa kazi; zimetolewa bure, na ni wazi zinatolewa na nani – kwa sababu katika mistari 9 tulioisoma, jina lake limetajwa mara tisa! Bila shaka ni Roho Mtakatifu ambaye anazitoa, na anaamua karama gani kumpa mtu gani. Paulo anataka tuone kwamba Roho Mtakatifu ndiye anayetoa karama hizi kwetu.

Sasa, ni muhimu kusema kwamba, kuna aina mbili za karama, ambazo watu wanazo: vipaji vya asili – na karama za Roho. Vipaji vya asili ni vile tulivyo kuwa navyo, kabla hatujawa Wakristo. Kila mmoja ana vipaji vya asili – tumezaliwa na vipaji hivyo – bila shaka vimetolewa na Mungu, ingawa watu wasio Wakristo hawawezi kutambua kwamba vipaji hivyo, vimetoka kwa Mungu. Na kwa hiyo, tunapokuwa Wakristo, tunaweza kuvitoa vipaji hivyo vya asili kwa Mungu, na kuvitumia katika kumtumikia. Lakini karama za Roho zinatolewa na Roho Mtakatifu kwa wote walio Wakristo tu. Na bila shaka, hilo linaleta maana – yejote asiyehiyo, hawezu kuwa na Roho Mtakatifu kwa kuwa

ye ye hakai ndani ya watu kama hao, na kwa hiyo hawatakuwa na karama za Roho. Kwa hiyo, kusudi la karama za Roho ni nini? Muhubiri wa Kimarekani John Piper anasema hivi: “*karama za Roho ni uwezo unaotolewa na Roho Mtakatifu, kuelezea imani kwa maneno au vitendo, kwa kuimarisha imani ya mtu mwingine*”. Kusudi la karama za Roho ni nini? “*Kwa kuimarisha imani ya mtu mwingine*”. Kwa maneno mengine – si zawadi yako ya kutunza kwa ajili yako mwenyewe; si kwa faida yako tu, lakini ni ya kutumika katika huduma ya kanisa; ni lazima itumike kwa kutia nguvu na kuwajenga waamini wengine katika imani yao.

Na ndio maana Paulo, anaendelea kuzungumzia kuhusu mwili, kuwa na sehemu nyingi katika sehemu ya sura hii iliyobaki. Kama waamini, sisi ni sehemu ya mwili mmoja, kanisa – lakini sisi sote tuna sehemu mbalimbali za kufanya; sisi sote tuna karama tofauti za kutumia. Paulo anasema kitu hicho hicho katika Warumi 12:5-6: Paulo anasema: “*Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viingo, kila mmoja kwa mwenzake, Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya neema mliyopewa*”. Halafu anaendelea kusema, kama umepewa karama ya unabii, itumie. Kama umepewa karama ya kufundisha, au kuhudumia au kuongoza, hakikisha unaitumia katika kanisa, ndio maana umepewa karama.

Kwa hiyo – ni wapi katika Agano Jipya karama hizi zimetajwa, na ziko ngapi? Zimeorodheshwa katika sura tatu tofauti – na mtaona nimeziorodheshwa katika notisi zenu. Na ingawaje idadi kadhaa za karama zimetajwa zaidi ya mara moja, nafikiri jumla ya karama mbalimbali inafikia 19, ingawa baadhi ya watu wanasema kwamba kuna zaidi ya hizo. Nizitaje:

Warumi 12:6-8: *unabii, huduma, kufundisha, kuonya, kukirimu, kusimamia, na kurehemu.*

1 Wakorintho 12:8-10: neno la hekima, neno la maarifa, imani, kuponya, miujiza, unabii, kupambanua roho, aina za lugha, na tafsiri za lugha. Na mstari 28: mitume, manabii, walimu, miujiza, karama za kuponya wagonjwa, masaidiano na maongozi, na aina za lugha.

Waefeso 4:11: Mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji, na walimu.

Na ninafikiri kwamba karama zilizoorodheshwa hapa, katika Waefeso, ni maalum kwa utumishi wa wakudumu, badala ya karama ambazo zinaweza kutumiwa na mwamini yeyote tu. Mara zote tutawaona watu wenye karama hizi, wakifanya kazi katika nafasi za kudumu katika kanisa, au masherika. Nina swali. Je, unajua karama zako za roho ni zipi?

Ngoja nisome mistari kadhaa katika 1 Wakorintho – na nafikiri ninapoisoma, ni rahisi kuona ushauri wa Paulo ukoje kwetu. Mwishoni mwa 1 Wakorintho 12:31 Paulo anasema hivi: “*takeni sana karama zilizo kuu*” – na halafu katika sura 14:1anatumia maneno sawasawa: “*ufuateni upendo na kutaka sana karama za rohoni, lakini zaidi kwamba mpate kuhutubu*”. Paulo anasema, sitaki muwe wajinga kuhusu karama za roho – lakini badala yake nataka mztake sana. Nataka mztake; nataka muwe na shauku kubwa kuhusu hizo, na nawataka mztamani sana. Na mtaona kwamba Paulo pia aliongeza maneno, “*hasa ‘karama kuu’*”, na ya kwamba anapendekeza kuwa baadhi ya karama ni kuu kuliko zingine – na anaivorodheshwa ‘*karama ya unabii*’ kuwa ni karama mojawapo ya karama kuu.

Sasa - sitaki kusema sana kuhusu karama hizi kuu, lakini nataka niseme neno la kuonya hapa – tunahitaji kuwa makini hapa. Walimu wa Biblia wanasema kwamba, mojawapo ya sababu za Paulo kuwaandikia kanisa la Wakorintho ni kwamba, baadhi ya Wakristo walitumia vibaya karama zao, na baadhi yao walikuwa wakijisifia. Labda baadhi yao walikuwa na karama hizi kuu ambazo Paulo anazizungumzia, lakini badala ya kuzitumia kwa njia ya unyenyekevu ili kuwatumikia wengine. Walianza kujifikiria wenyewe kama ni muhumi zaidi katika kanisa; walifikiri wana hadhi ya juu kuliko wengine. Ingawaje wewe ni mchungaji katika kanisa, hilo halikufanyi kuwa muhumu zaidi, kuliko mtu

mwingine yeyote yule katika kanisa. Labda - umepewa karama kuu, lakini haimaanishi kwamba wewe ni bora kuliko mtu mwingine yeyote. Haimaanishi kwamba wewe ni maalum zaidi.

Tuangalie Warumi 12 na sehemu ambayo Paulo anazungumzia karama za Roho, kwa sababu Paulo ana maneno kadhaa muhimu sana kuwaambia watu wote kanisani, ambao wanajifanya kama wao ni muhimu kuliko wengine. Tuangalie katika mstari 3: “*Kwa maana kwa neema niliyopewa, namwambia kila mtu aliyeo kwenu, asinie makuu kupita ilivyompasa kunia; bali awe na nia ya kiasi, kama Mungu alivyomgawia kila mtu kiasi cha imani*”. Paulo anaendelea kuzungumzia karama mbalimbali, ambazo watu walio kanisani wanazo. Na anasema, usijifikirie mwenyewe sana – usijikuze kwa sababu ya karama fulani ambayo Mungu amekupa. Tuangalie katika Wafilipi 2:3-7: “*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Yesu Kristo*”. Ingawaje wewe ni kiongozi wa kanisa; kama wewe ni kiongozi wa makanisa matano; kama wewe una karama za Roho, 1, 2, 3, au 4; hata kama una mojawapo ya karama kuu: uwe mnyenyekuvu. Kumbuka kwamba karama hizi zimetolewa bure na Roho Mtakatifu kama anavyoamua, na kumbuka kwamba ni lazima zitumike katika kuhudumia wengine kanisani.

Nina maswali machache kwenu. 1. Je, unajua karama zako za roho ni zipi? 2. Je, unatumia karama zako ambazo umepewa kwa faida ya wengine? 3. Je, unatamani sana karama za roho? Sasa, wewe tu mwenyewe unaweza kujibu maswali hayo – ni wewe tu. Ngoja niseme maneno machache tu kuhusu kutafuta zaidi karama za Roho katika maisha yetu – nafikiri jibu ni rahisi sana, lakini linahitaji kama maelezo 3. Ningeweza kusema kwamba, kama unatamani sana karama za Roho, uje mbele za Mungu kwa maombi, ukimsihi akupe karama kupitia Roho Mtakatifu, na si kuombea mara moja tu, na kusahau kuhusu hilo, lakini uendelee kuombea. Lakini – na hapa ndipo panapo hitaji kuwa na maelezo kadhaa.

1: Nafikiri kwamba imetupasa kuhakikisha kwamba tayari tunatumia karama alizotupa, kabla hatujaomba zaidi. Kwa nini Mungu atupe karama zaidi, kama hatutumii zile ambazo amesha tupa? Kuna watu ambao hawatumii karama zao. Fikiria wazazi wangejisikiaje kama wangempa mtoto wao zawadi nzuri sana. Waliifunga zawadi kwa uangalifu, na halafu walimpa mtoto. Na mtoto aliichukua na kusema ‘*asante sana*’ – lakini badala ya kuifungua aliiweka sakafuni, na aliondoka kufanya mambo mengine! Hata hakufungua zawadi ili aone ikoje! Kwa njia hiyo hiyo, fikiria kuhusu Roho Mtakatifu anajisikiaje, wakati ambapo ametupa zawadi hatuzitumii, na bado hatujachukua muda au nafasi ya kutaka kujua ni nini, na hatujazitumia kuhudumia wengine.

2. Pia nafikiri kwamba tunahitaji kuomba kwa nia nzuri. Kama tunaomba karama kwa sababu tunafikiri itatufanya tuonekane wazuri kanisani, hiyo ni kwa sababu ya ubinagsi, na maombi yetu hayatajibowi. Baadhi ya watu kanisani wanataka kujisifu kuhusu karama zao, na hiyo ndiyo ilikuwa chanzo cha shida katika kanisa la Korintho. Na Paulo alikuwa lazima awaandikie barua kuwaambia jinsi ya kutumia karama zao kwa usahihi. Kwa hiyo, tusiombe kwa nia ya ubinagsi. Kisha, namba 3: pia tutambue kwamba Roho Mtakatifu ambaye anaamua nani apokee karama gani (1 Wakorintho 12:11). Tunaweza kuomba karama fulani, lakini lazima tukubali kwamba Roho Mtakatifu anajua vizuri, na hawezi kutupokea maombi yetu.

Kwa hiyo, ngoja nimalize kwa neno la kutia moyo kutoka kitabu cha 1 Petro 4:10: Petro anasema hivi: “*Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu.*” Tusiwe wajinga kuhusu karama za Roho. Muwe macho mkijua kwamba kila Mkristo wa kweli amepewa angalau karama moja ya rohoni. Hatuzistahili, lakini karama hizo zimetolewa bure na Roho Mtakatifu – kwa nini? Kwa faida ya kanisa – kwa ajili ya Wakristo wengine – kwa ajili ya kaka na dada zetu katika Kristo – lazima tuzitumie kuimarisha kanisa, na si kwa sababu za ubinagsi. Kwa hiyo, “*Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana*”.

## KIPINDI 7 – MASWALI

1. Unafikiri kuna karama za Roho siku hizi? Kwa nini?
2. Utambua zawadi/vipaji vyako vya asili? Zikoje?
3. Unazijua karama zako za rohoni? Ni zipi?
4. Je unatumia karama zako kuimarisha kanisa? Unaweza kuzitumia zaidi?
5. Kuna karama ngapi za Roho zimetajwa katika Agano Jipy?
6. Je huwa unatamani kuwa na karama za Roho zaidi? Ungependa karama gani uwe nayo ambayo sasa huna?
7. Tatizo katika kanisa la Korintho likuwaje?

## KIPINDI CHA 8: KUNENA KWA LUGHA

Tunakwenda kuendelea na mada ya karama za Roho, lakini nataka tulenge juu ya zawadi moja pekee – na hiyo ni karama ya kunena kwa lugha. Hii mara kwa mara imekuwa mada inayoleta mabishano makali, hasa katika makanisa yale ambayo si ya Kipentekoste au ‘*kikarismatiki*’, lakini kwa kweli, hakuna taarifa nyingi katika Biblia kuhusu karama hii maalum. Kwa kushangaza imetajwa mara moja tu katika Injili – katika sura ya mwisho ya Marko (16:17), na mara tatu tu katika kitabu cha Matendo – na kwa hiyo, labda si muhimu kama baadhi ya watu wanavyofikiri. Imeorozeshwa kama karama ya Roho katika 1 Wakorintho 12 – lakini haijaorozeshwa katika Warumi au Waefeso, ingawaje Paulo amezungumzia sana kuhusu hilo katika 1 Wakorintho 14. Kwa kweli imetajwa mara 16 katika sura hiyo, na hapa ndipo tunapopata taarifa zetu zaidi kuhusu mada hii.

Kirai kilichotumika katika Biblia ya Tafsiri ya Union ni ‘*kunena kwa lugha*’, lakini katika makanisa mbalimbali, na tafsiri nyingine za Biblia, kirai kinachotumika ni ‘*kunena kwa ndimi*’. Vyote viko sawa, lakini labda kirai ‘*kunena kwa ndimi*’ kimesikika kikileta mabishano zaidi ya vingine! Neno la Kigiriki ambalo limetumika kwa karama hii ya roho, ni “*glossolalia*”, ambalo hasa kimsingi ni ‘*ulimi*’ au ‘*lugha*’. Kabla hatujaangalia 1 Wakorintho 14, turudi nyuma kwenye Matendo 2 na kuangalia tena nini kilichotokea katika Siku ya Pentekoste. Tuangalie Matendo 2:4-8:

Na kwa hiyo, ni nini ‘*kunena kwa lugha*’? Hii ni pointi namba 1: Katika Siku ya Pentekoste ilionekana bila shaka kwamba, wanafunzi waliongea kwa lugha nyingine ambazo zilitambulikana kwa watu wengine. Kilichotoka vinywani mwao ni lugha zilijulikana – lakini hazikujulikana kwa wanafunzi. Wasikilizaji walitambua lugha zao wenywewe, lakini wanafunzi hawakuelewa walichokisema. Hawakujifunza lugha ambayo walizungumza, na hawakuwa wamezitumia kabla ya hapo. Alikuwa ni Roho Mtakatifu aliywawezesha kuongea kwa njia hiyo. Unaweza kutafakari ilivyo kuwa kwa wanafunzi hawa, ghafla, kuanza kuongea lugha ambayo hawajajifunza? Hebu tafakari kama ni wewe unaanza kuongea kwa ufasaha katika Kifaransa au Kirusi au Kiarabu au Kichina – nina hakika ungeshangazwa! Na hivyo ndivyo ilivyotokea katika siku hiyo ya Pentekoste.

Wanafunzi walikuwa wanaongea kwa lugha zinazojulikana – na ninafikiri tunaweza kusema vile vile kwa marejeo mengine mawili, katika kitabu cha Matendo, na nimeyao rodhesha katika notisi zenu. Katika matukio yote matatu, watu walibatizwa na kujazwa Roho Mtakatifu, na kwa sababu hii, walikuwa wamewezeshwa kuongea kwa lugha hizi – hii ni karama waliyopewa na Roho Mtakatifu. Kwa hiyo – pointi namba 1: katika kitabu cha Matendo, ingeonekana kwamba watu waliponena kwa lugha; walinenwa kwa lugha inayotambulika.

Lakini, tuangalie 1 Wakorintho 14, na hii ndiyo pointi namba 2: tunapofika katika kitabu hiki, inaonekana kwamba kunena kwa lugha inachukua maana nyingine, kwa sababu inahusisha lugha ambazo hazijulikani au hazitambulikani kwa wengine. Kwa nini na sema hivi? Tazama mstari 2: “*Maana yeye anenaye kwa lugha (au ndimi), hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye; lakini anena mambo ya siri katika roho yake*”. Hapa, inaonekana kwamba hakuna anayeelewa lugha ambayo imekuwa ikizungumzwa – msemaji anazungumza kwa Mungu kwa maombi na sifa; anaongea kwa silabi ambazo hazieleweki kwa msemaji; bali kwa Mungu pekee. Ni lugha takatifu; lugha ya mbinguni; labda huenda ikawa ni lugha ya malaika. Kwa kweli, angalia katika 1 Wakorintho 13:1: Paulo anasema: “*Nijaposema kwa lugha za wanadamu - na za malaika*”. Kwa hiyo, labda, kunena kwa lugha ni lugha ya mbinguni.

Pointi namba 3: Nini kinatokea mtu anaponena kwa lugha? Nini kinatokea wanaponena kwa lugha ya mbinguni ambayo hawailewi? Kusudi ni nini? Tuangalie 1 Wakorintho wa Kwanza 14:4: Paulo anasema hivi: “*Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake*”. Anajielimisha mwenyewe; anajijenga mwenyewe kwa sababu kinachotokea ndani yake; anajitia moyo mwenyewe. Haelewi anachokisema, kwa hiyo akili yake haifundishwi – lakini ndani ya roho yake, kuna hisia kali ambayo inaongea na Mungu, na hisia zeny shauku, na kujitolea kwa namna ya ajabu kwa Mungu akikua ndani.

Pointi namba 4: Je, ni lazima Wakristo wote wanene kwa lugha? Tuangalie mstari 5. Hivi ndivyo Paulo anvyosema: “*Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha, lakini zaidi sana mpate kuhutubu*”. Je, ni lazima Wakristo wote wanene kwa lugha? Kuna baadhi ya watu wanaosema kwamba kila Mkristo lazima anene kwa lugha. Nafikiri watu kutoka kanisa la Kipentekoste wangesema hivi. Kiukweli utakuta watu wanaosema kwamba, kama mtu haneni kwa lugha, yeye hata si Mkristo. Ninapingana na hilo – ninafikiri mtazamo huo si sahihi, na ninafikiri kwamba shida nyingi zilisababishwa wakati uliopita, kwa sababu ya mtazamo huo. Lakini unaposoma mstari 5, nafikiri ni dhahiri Paulo alichosema. Angalia tena: “*nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha*”. Paulo anasema, ‘*natamani kwamba ninyi nyote mngepata uzoefu wa lugha ya mbinguni, kwa sababu ni hisia ya ajabu, na inayomjenga na kumtia moyo mtu katika kutembea kwake na Bwana*’.

Tafadhali zingatia - hasemi ‘*ninyi nyote lazima mnene kwa lugha*’ – anasema ingekuwa vizuri kila moja angepata karama hii – lakini anajua kwamba si kila mmoja anayo. Na sababu ya kusema hivyo ni kwamba, ni kwa sababu ya kile alichosema katika 1 Wakorintho wa Kwanza 12. Tunajua kwamba kunena kwa lugha ni karama ya Roho, inayotolewa na Roho Mtakatifu – lakini kama ukiaangalia 12:30, utaona kwamba Paulo anadokeza kwamba si kila mmoja atanena kwa lugha. Paulo anasema hivi katika mstari 30: “*Wote wana karama za kuponya wagonjwa? Wote wanena kwa lugha? Wote wafasiri?*” Jibu ambalo anatutaka tutoe kwa maswali hayo ni ‘*hapana, si kila mmoja ana karama hizi*’. Si kila mmoja ana karama za kuponya wagonjwa – kama wangekuwepo kusingekuwa na wagonjwa hata mmoja duniani! Na si kila mmoja ana karama ya kunena kwa lugha. Wote tumepewa karama tofauti, kama Roho Mtakatifu anavyoamua. Na kwa hiyo, kama mtu anakuja kwako na kusema “*lazima unene kwa lugha*” unaweza kumwonyesha mstari huu!

Turudi katika sura 14, kwa sababu ninatambua kwamba Paulo ametaja neno ‘*unabii*’ katika mstari 5. Paulo anasema kwamba angependa watu waweze kutoa unabii kuliko kunena kwa lugha – kwa nini? Jibu liko kwenye mstari 4: Kwa sababu anayetoa unabii anawenza kujenga na kutia moyo kanisa zima – lakini mtu anayenena kwa lugha hujijenga mwenyewe tu – ndiyo maana Paulo anaiona karama ya unabii kuwa ni karama kuu kuliko karama ya lugha. Lakini, ni nini hasa karama ya ‘*unabii*’? ‘*Unabii*’ katika Agano la Kale unamhusisha Mungu akiongea moja kwa moja kwa nabii, naye nabii analeta taarifa hizi kwa watu – kwa hiyo nabii angesema na watu “*hivi ndivyo Bwana anavyosema*”. Katika Agano Jipy, na katika kanisa leo, ‘*unabii*’ unaonekana kuwa tofauti. Labda unajumuisha utabiri kuhusu wakati ujao. Labda unajumuisha mahubiri yenye nguvu, kunena neno la Mungu – lakini mara kwa mara ‘*unabii*’ leo unaonekana kumhusisha maneno kutoka kwa Mungu, aliopewa mtu fulani

*kwa kuliimarisha kanisa. Labda ni ujumbe au onyo ambalo Mungu ameliweka katika akili ya mtu, katika njia hiyo mtu huyo anahisia kwamba ujumbe huo kwa hakika umetoka kwa Mungu.*  
*Katika 1 Wakorintho 14:29-32 Paulo anazumgumza zaidi kuhusu ‘unabii’, na labda baadaye, unaweza kusoma mistari hii. Hiyo ilikuwa pointi namba 4: Je, ni lazima Wakristo wote wanene kwa lugha? Binafsi sifikiri kwamba kila Mkristo ana karama ya kunena kwa lugha.*

Pointi namba 5: ni fupi sana. Tuangalie katika 1 Wakorintho 14:13: “Yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kufasiri”. Na halafu, Paulo anaendelea kusema kwamba yeze anaposema, au kuomba au kuimba kwa lugha, akili yake haina matunda – haelewi anacho sema; na kwa hiyo mtu ambaye ananena kwa lugha ni lazima aombe karama ya kufasiri. Ni lazima aombe kwamba pia aelewé lugha ya mlbinguni katika kunena kwake.

Pointi namba 6: Namna gani kuhusu matumizi ya karama ya kunena kwa Lugha katika kanisa? Tuangalie katika 1 Wakorintho 14:27-28: “*Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu, na mmoja na afasiri. Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na anyamaze katika kanisa; aseme na nafsi yake tena na Mungu*”. Inaonekana kwamba Paulo anaweka masharti 3 kwa matumizi ya kunena kwa lugha katika kanisa. 1. Watu 2 au 3 tu wafanye hivyo katika kusanyiko. 2. Watu hao wafanye hivyo kwa kupeana zamu, si kwa muda huo huo. Na 3. *Kuwe na mfasiri. Kwa maneno mengine, kama hakuna mtu katika kanisa ambaye ana karama ya kufasiri, inaonekana kwamba karama ya kunena kwa lugha isitumike kwa sauti katika ibada, lakini itumike kwa mtu binafsi. Paulo anasema wakae kimya kanisani, na waongee wao wenyewe na Mungu.*

Ngoja niseme kitu fulani hapa, ambacho nafikiri ni muhimu. Kama tutaangalia mistari hiyo miwili kwa makini, tutagundua kwamba mtu ambaye ana karama ya kunena kwa lugha, anaweza kudhibiti karama yake. Anaweza kuanza na konyamaza anapoamua. Tunaweza kuona haya katika mstari 27 na 28. Paulo anasema “*waseme zamu kwa zamu*”, na ‘anyamaze’ kama hakuna mfasiri. Hili linapendekeza wanaweza kuamua lini, na wapi, wanene kwa lugha. Watu wengi wanafikiri kwamba kama mtu ana karama ya kunena kwa lugha – hawawezi kudhibiti wanachosema; maneno hayo yana miminika tu kutoka katika midomo yao, na hawawezi kuyazuia yasitoke. Wanafikiri ni mazungumzo ambayo hayawezi kudhi-bitwa. Hiyo si kweli.

Na ninafikiri kwamba Paulo, anaonyesha hivyo hapa kwenye mistari hii. Kwa kweli angalia mstari 32: Sasa, najua kwamba hapa Paulo anarejelea ‘*manabii*’, lakini pia nafikiri inawahu wale wote ambao wanaweza kunena kwa lugha. Kuna kufanana kwingi kati ya mambo haya mawili, kwa sababu watu wanaweza kutabiri kwa kunena kwa lugha. Unasemaje? Mstari 32: “*roho za manabii huwatii manabii*”. Angalia kwa makini, kwa sababu utaona kwamba neno ‘*roho*’ limeandikwa kwa herufi ndogo ‘r’, ambayo maana yake inaonyesha roho ya mtu, si Roho Mtakatifu. Ngoja niwasomeeni mstari huo, kwa tafsiri nyingine ili kuweka wazi zaidi kile kilichosemwa hapa. Tafsiri ya Maisha Mapya ni tafsiri ya kisasa. Hivi ndivyo inavyosema: “*Kumbuka watu ambao wanatabiri wanazidhibiti roho zao, na wanaweza kusubiri zamu yao*”.

Na ni vile vile kwa watu ambao wanenena kwa Lugha. Wanaweza kudhibiti wanapofanya hivyo. Hawashindwi kudhibiti kunena kwao – au labda niseme, wasishindwe kudhibiti kunena kwao! Unaona, moja ya sababu ambayo inamfanya Paulo kuandika barua hii kwa Wakristo wa Korintho, ni kwa sababu karama za roho zilikuwa zinatumika vibaya. Inaonekana kwamba kanisa lilipokusanyika pamoja kwa ibada, kila mmoja alitaka kuongea, na kila mmoja alitaka kusikika, na kwa hiyo watu wengi walianza kutabiri na kunena kwa lugha kwa pamoja – na matokeo yake ilikuwa ni kelele na machafuko. Na kwa hiyo, Paulo anawaambia, katika mstari 20 – ninyi nyote mmepewa karama tofauti na Roho Mtakatifu; acheni kujisifu; acheni kuwa wabinafsi, na acheni kufikiri kwamba ninyi ni muhimlu zaidi kuliko mtu mwingine yejote. Paulo anawakaripia hapa! Unaona, karama za Roho

zinapokuwa zinatumika kanisani, daima patakuwa na watu wachache ambao wanazitumia vibaya, na hicho ndicho kilichotokea katika kanisa la Korintho.

Na hivyo ndivyo inavyotokea katika makanisa mengi siku hizi. Baadhi ya watu wanatumia karama zao vizuri, na kanisa linabarikiwa - lakini baadhi ya watu wanazitumia vibaya karama zao. Na kwa hiyo tunahitaji kuwa makini. Kwa hiyo, pointi 6: Mtu ye yote mwenye karama ya kunena kwa lugha anaweza kudhibiti kamara hiyo. Na kama hakuna mtu kanisani anayeweza kufasiri lugha, karama ya kunena kwa lugha isitumike kanisani, bali iwe kwa matumizi binafsi tu.

Hatimaye, pointi namba 7. Ingawa baadhi ya watu wanatumia vibaya karama za Roho, na ingawa baadhi ya watu wanatumia vibaya karama ya kunena kwa lugha, hilo halimaanishi, kwamba imetupasa kuzuia matumizi sahihi ya karama za Roho, katika makanisa yetu. Tuangalie mstari 39: "*msizue kunena kwa lugha*". Nafikiri ni dhahiri kile Paulo anasema - haihitaji maelezo yeyote. Msizue karama hii katika kanisa lenu; msiache wala kuizua, lakini hakikisheni inafanyika katika njia sahihi. Angalia Paulo anavyosema katika mstari 33, na mstari 40. Anazungumzia kuhusu utaratibu katika kanisa. Mstari 33: "*Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko bali wa amani*", halafu tazama mstari 40: "*mambo yote yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu*".

Kwa hiyo – tumetumia muda mwingi kuangalia karama hiyo moja, lakini nafikiri ni somo muhimu, na kwa hiyo natumaini, baada ya kuwa timesoma 1 Wakorintho 14 kwa kina, tutakuwa tumeongeza uelewa mzuri juu ya karama hii. Na tunapofunga mukutano huu – na tunapomaliza mafundisha yetu kuhusu Roho Mtakatifu; tuangalie 1 Wathesalonike 5:19 unasema hivi: "*Msimzimishe Roho*".

Msimgandamize Roho Mtakatifu katika maisha yenu, au katika kanisa lenu. Msimpuuze, lakini mumkaribishe katika maisha yenu; na kumruhusu atawale maisha yenu. Uhusiano wenu na Yesu utakua, na utumishi wenu utakuwa wa kufaa zaidi.

## KIPINDI 8 – MASWALI

1. Ni mara ngapi kunena kwa lugha kumetajwa katika Injili?
2. Kitabu gani na sura gani katika Agano Jipy huzungumzia zaidi juu ya suala la kunena kwa lugha?
3. Kuna tofauti gani kati ya karama ya kunena kwa lugha katika siku ya Pentekoste na karama ya kunena kwa lugha katika Kitabu cha Wakorintho wa Kwanza?
4. Kitu gani hutokea mtu anaponena kwa lugha?
5. Je, ni lazima Wakristo wote wanene kwa lugha? Kwa nini ndiyo au ni hapana?
6. Kwa nini unabii ni mojawapo ya karama kuu?
7. Je, ni lazima watu wanene kwa lugha kanisani siku hizi? Kwa nini ndiyo au kwa nini hapana?

### Maelezo ya Ziada - Kipindi cha 8:

Si kila moja atakobaliana na nilichokuwa ninakifundisha leo, au katika siku chache zilizopita. Kuna watu wengi katika kanisa ambao hawaamini kwamba watu wanaweza kweli kunena kwa lugha siku hizi. Wanafikiri kwamba wale wote ambao wanadai kufanya hivyo, wanaongea maneno yasio na maana lambayo wamejifunza au ikuyatengeneza tu. Na pia kuna watu ambao wanasema kwamba karama nyininge za miujiza za Roho Mtakatifu hazifanyi kazi siku hizi. Wanasema kwamba Mungu hafanyi kazi kwa njia ya wazi na njia ya kimiujiza, kama alivyofanya katika kanisa la Agano Jipy – na kwa hiyo, inamaanisha hawaamini kwamba miujiza, uponyaji, unabii, na kunena kwa lugha, inatokea siku hizi. Neno linalotumika kwa mtu anayeamin hivi, ni "*cessationist*". Neno hilo lina maana gani? Linarejelea kitu ambacho kimemalizika au kwisha.

Wanaamini kwamba, karama za miujiza zilikoma Mitume walipokufa, au miaka mia mbili baada ya kuanza kwa kanisa. Wanakubali kwamba Roho Mtakatifu alikuwa mtendaji katika kanisa la kwanza,

na karama hii ilitolewa na kutekelezwa katika miaka hiyo ya mwanzo – lakini wangesema hiyo ilitolewa kuzindua Ukristo, na kulipa kanisa mamlaka kadhaa, lakini mara kanisa lilipoanzishwa, hakuna hitaji lolote la nguvu za kiroho, na kwa hiyo, wanasema Roho Mtakatifu alirudi nyuma, na hajionyeshi tena kwa njia hiyo ambayo aliitumia. Bado wanaamini kwamba Roho Mtakatifu anafanya kazi katika maisha ya Mkristo leo – lakini si kwa njia aliyofanya katika kanisa la kwanza.

Lazima ni seme, na haya ni maoni yangu mwenyewe, nafikiri kwamba mtazamo unamokosa, na sifikiri kwamba kuna jambo lolote katika Biblia kinalosema kwamba karama za roho zimeondolewa siku hizi. Na ninafikiri kwamba, kama watu wamechagua kufutilia mbali ishara, na maajabu na miujiza leo, wanafuta wingi wa maneno ambayo Agano Jipya lilikuwa liseme kwetu. Na pia hawajali shughuli za Roho Mtakatifu duniani kote leo. Pia naamini kwamba mtazamo huu unamzimisha na kumhuzunisha Roho Mtakatifu. Katika 1 Wathesalonike 5:19 unasema hivi: “*Msimzimishe Roho*”. Msimgandamize Roho Mtakatifu katika maisha yenu, au katika kanisa lenu, na msimwekee mipaka kwa mambo ambayo Roho anaweza kufanya.